# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Julai 14, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581737

www.ippmedia.com

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com




UKURASA WA 4
**Udanganyifu** wapungua, Hisabati bado maumivu kitaifa



UKURASA WA 5
**Watoto** kunajisiwa kisha kuuawa, polisi wawatia mbaroni wawili

UKURASA WA 17
**Uchunguzi** maiti zilizokatwakatwa, kufungwa katika viroba waanza

**ARGENTINA, COLOMBIA KITACHIMBIKA**
UKURASA 22

# Mafao yanavyovuruga ndoa, kuchochea vifo

• **Mume,** mke wastaafu pamoja, mke aficha milioni 120 zake, pensheni ya mwezi... *Endelea ukurasa 11*



UKURASA WA 2
## DK. MPANGO ANG'AKA RUSHWA KITUO CHA AFYA



MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amemtaka Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Isack Mwakisu kutumia vyombo vya ulinzi na...

UKURASA WA 11
## KUNA KITU NDANI YA HOJA YA LEMA WA CHADEMA



Linganisha masuala ya uchumi, kuongezeka kwa makali ya gharama za maisha, mahitaji ya ajira, kipato duni au kupaa kwa bei za bidhaa...

UKURASA WA 18
## MAMBO YA FARAGHA SASA HADHARANI



TAIFA lolote lisilojengwa katika misingi ya maadili mema ni rahisi...

## Mwinyi: Kodi na tozo ziondolewe bidhaa za mkakati

UKURASA 3



## Samia ashusha kibano vigogo wa wizara nne

UKURASA 2

MICHEZO 'NATAKA YANGA IWE YA TANO BORA AFRIKA' UK.24 KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Mpango ang'aka madai ya rushwa kituo cha afya, aagiza uchunguzi

**Na Mwandishi Wetu,** KASULU

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amemtaka Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Isack Mwakisu kutumia vyombo vya ulinzi na usalama kuchunguza malalamiko ya wajawazito kuombwa rushwa katika Kituo cha Afya Makere, Halmashauri ya Mji wa Kasulu.

Dk. Mpango alitoa maagizo hayo wakati akiwa katika Mji wa Makere baada ya kupokea malalamiko ya wananchi dhidi ya vitendo vya baadhi ya watumishi wa kituo hicho kuomba rushwa kwa wajawazito ili kuwapa huduma.

"Mkuu wa Wilaya una vyombo vinavyohusika na uchunguzi, hivyo unaposikia malalamiko ya wananchi elekeza vyombo vifanye uchunguzi ili uchukue hatua stahiki kwa watakaobainika, lakini msiwaonee," aliagiza Dk. Mpango.

Eva Moshi, mmoja wa wananchi waliopewa fursa kuzungumzia changamoto zinazowakabili, alidai mjamzito anapokwenda kujifungua katika kituo hicho, kama hana Sh. 50,000 hatopata kadi ya kliniki na atajifungulia nje.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Zainab Katimba, alisema ofisi yake itachukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtumishi yeyote atakayebainika kutoza mjamzito Sh. 50,000 kwa kisingizio cha kushindwa kufika kwa wakati katika kituo cha afya au zahanati.

"Kwa niaba ya Waziri Mohamed Mchengerwa, ninatoa maelekezo kwa watumishi wote wa kada ya afya kutimiza wajibu wao kikamilifu na kwa wale watakaoainika kuomba rushwa, hatua zitachukuliwa dhidi yao," alionya.

Mke wa Makamu wa Rais, Mama Mbonimpaye Mpango, alishukuru Naibu Waziri Zainab kwa kuahidi kutatua changamoto zinazokabili wananchi na kupongeza waliosema hadharani changamoto zinazowakabili ili zitatuliwe.

Dk. Mpango yuko katika ziara ya kikazi mkoani Kigoma kukagua utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akikagua mabanda mbalimbali ya maonyesho katika kilele cha Wiki ya Wazazi Kitaifa kwenye viwanja vya Azimio, wilayani Mpanda mkoani Katavi jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu CCM, Fadhili Maganya. **PICHA: IKULU**

# Rais Samia abana vigogo wizara nne

**Na Neema Hussein, Katavi**

VIGOGO katika wizara nne wamewekwa 'kitanzini' Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza wizara zao zikamilishe miradi zinayotekeleza ili kutoa huduma kwa wananchi.

Ameagiza Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha hadi mwezi Septemba mwaka huu, mradi wa ujenzi wa kituo cha kupokea umeme wa Sh. bilioni 48 na ule wa njia ya kupitisha umeme kwenda Gridi ya Taifa kutoka Tabora hadi Katavi unaogharimu Sh. bilioni 116 inakamilika.

Pia ameagiza Wizara ya Ujenzi kuhakikisha barabara zote zinazojengwa zikamilike kwa haraka na zile zinazotakiwa kuanza utekelezaji zifanyiwe kazi haraka.

Rais Samia alitoa maagizo hayo jana wakati akihutubia wananchi wa Wilaya ya Mlele, mkoani hapa, akielekeza mradi huo wa umeme ukamilike ndani ya muda huo ili wananchi wapate umeme wa uhakika.

Pia aliagiza Wizara ya Habari na Mawasiliano kuimarisha mawasiliano katika maeneo mkoa huo kwa kuwa wananchi wasipopata taarifa sahihi hawawezi kupata uelewa kuhusu serikali yao na yanayofanywa na serikali hiyo.

Katika ziara hiyo, Rais Samia jana alitembelea na kukagua miradi wa ujenzi wa kituo cha kupokea umeme wa Gridi ya Taifa cha Mlele kutoka Tabora hadi Katavi ambao umefikia asilimia 97 ya ujenzi wake.

Alisema mradi huo utakapokamilika utakuwa suluhisho la kukatikatika kwa umeme katika mkoa huo.

"Tangu nchi ipate uhuru, mkoa huu ulikuwa haujaunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa, gharama zinazotumika katika kuzalisha umeme kwa kutumia jenereta ni kubwa kwani kila mwezi mkoa huo unatumia zaidi ya Sh. bilioni mbili katika kuzalisha umeme unaosambazwa kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi.

"Nipo hapa Katavi kwa ziara ya kikazi na kichama, nikiwa hapa nitatembelea miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa, na asubuhi nimekagua kituo cha kupokea umeme Gridi ya Taifa kilichopo hapa Mlele.

"Nimeona kazi nzuri inayofanyika, hii tunatekeleza Ilani cha Uhaguzi ambayo tuliahidi kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa wananchi," alisema.

Rais Samia aliomba wananchi kuchangamkia fursa za uwekezaji zinazotokana na kupata umeme wa Gridi ya Taifa na kulipia gharama za umeme kutokana na matumizi wanayotumia.

Mkuu wa Nchi pia alishukuru wananchi waliotoa maeneo yao kupisha mradi ambao wanasubiri kulipwa fidia na kusisitiza kuwa watu wote ambao wamepitiwa na mradi watalipwa fedha zao zote kwa kuwa kuna Sh. bilioni nne zilizotengwa kwa ajili yao.

Rais Samia alisema Wizara ya Ujenzi imefanya kazi kubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara ambapo barabara kutoka Tabora hadi Katavi imekamilika kwa kiwango cha lami.

Alisema serikali inatarajia kuanza ujenzi wa barabara ya Kibaoni-Makutano ya Mlele ambayo ni kilomita 50, Vikongwe-Uhavywe kilomita 25, Luhavywe-Mishamo zaidi ya kilomita 37 na Kakwira-Kalema kilomita 110 ambazo zitajengwa kwa kiwango cha lami na fedha zipo.

"Nimefurahishwa na kazi inayofanywa na Wizara ya Ujenzi kwani barabara kutoka Tabora- Mpanda ni mkeka tu, nimepita mpaka nikasinzia, haya ni maendeleo makubwa sana.

"Pamoja na hayo serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya barabara, tunataka mkoa huu tuunganishe kwa lami maeneo yote ili kurahisisha ukuaji uchumi wa mkoa huu.

"Ninaagiza Wizara ya Ujenzi kuhakikisha barabara zote zinazojengwa zikamilike haraka na zile ambazo zinatakiwa kuanza utekelezaji wake mzifanyie kazi haraka ili mkoa huu uunganishwe na lami pande zote," aliagiza.

Rais Samia pia alisema amepokea maombi ya Mbunge wa Katavi, Issack Kamwelwe, kuhusu wananchi wa jimbo hilo kupewa maeneo ya kulima na kufuga katika Hifadhi ya Taifa Katavi.

"Nimepokea maombi ya mbunge wenu na yatafanyiwa kazi na bahati nzuri Waziri wa Maliasili yupo hapa. Ninachoomba wananchi wa mkoa huu na nchi nzima kuendelea kutunza na kuhifadhi mazingira.

"Tunafahamu kuna uhaba wa ardhi kulingana na idadi ya watu. Watu wa mkoa huu mmebarikiwa kuzaa, lakini uhaba wa ardhi usiwe chanzo cha kuharibu mazingira ya hifadhi zetu.

"Kinachotakiwa ni kukaa na serikali na kuangalia mahitaji ya watu, basi tunachukua hatua ya kukata eneo la hifadhi ili wafanye shughuli za kilimo na ufugaji," alisema.

Alionya viongozi wasihamasishe wananchi kuvunja sheria, baadaye kuwa mstari wa mbele kutetea wanaochukuliwa hatua kutonana na uvunjaji sheria.

Alisema serikali itajenga minara ili usikivu wa vyombo vya habari uwe rahisi kwa kuwa "jamii yenye taarifa ndiyo inaweza kufanya uamuzi sahihi".

HABARI KITAIFA

# Mwinyi: Bidhaa za kimkakati ziondolewe kodi, tozo nchini

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussen Ali Mwinyi amezitaka mamlaka zinazohusika katika biashara na uwekezaji kwa pande zote za muungano, ziondoe urasimu na kuwezesha zaidi biashara.

Pia amezitaka kupunguza gharama za bidhaa kwa kuondoa kodi na tozo kwenye maeneo na bidhaa za kimkakati.

"Serikali zote mbili zitaendelea kuhamasisha biashara na uwekezaji zaidi katika maeneo ya kimkakati ili kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa na kuboresha mazingira ya biashara ambayo yatanufaisha wananchi wetu.

"Serikali zote mbili zina nia thabiti kuboresha mazingira ya biashara na kwa kuelekeza taasisi za serikali kusomana katika mfumo, kupunguza gharama za bidhaa na kuondoa kodi na tozo kwenye maeneo ya kimkakati," alisema Rais Mwinyi jana mkoani Dar es Salaam.

Rais Mwinyi aliyasema hayo wakati akifunga Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam , maarufu Sabasaba, aliyoyataja ni nyenzo muhimu kwa ukuaji wa biashara nchini.

Pia alizitaka taasisi hizo zenye mamlaka na biashara kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi ili kuongeza fedha za kigeni nchini.

Alisema kwa sasa kuna fursa kubwa ya masoko, ikiwamo soko huru la Afrika, soko la Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambayo wigo wake umeongezeka na kutoa fursa ya kufanya biashara miongoni mwa nchi za Bara la Afrika lenye jumuiya nane na nchi 54.

"Hivyo, TanTrade fanyeni utafiti wa uhakika na uchambuzi wa fursa ziliziko katika masoko hayo ambako bidhaa zetu zinaweza kwenda na kutoa taarifa hizo kwa wafanyabiadhara wetu nchini," aliagiza.

Rais Mwinyi pia alitoa wito kwa wafanyabiashara kutumia vizuri wafanyabiashara wenzao waliowapata (wa ndani na nje) katika maonesho hayo.

Pia aliwataka kuongeza uzalishaji bidhaa ambazo zina mahitaji makubwa katika masoko ya ndani na nje hususani sukari, mafuta ya kupikia, bidhaa za mwani, unga wa ngano, bidhaa za ujenzi, dagaa na samaki.

"Nimefurahishwa na mabadiliko ya maonesho ya mwaka huu, nimeshuhudia hilo katika mabanda nilikopita, kuna kila sababu ya kupongeza mamlaka zilizohusika kuandaa," alisifu Rais Dk. Mwinyi.

Waziri Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaban, alisema wizara yake inayatumia maonesho hayo kama fursa kwa wajasiriamali kutafuta na kutengeneza mtandao wa biashara ndani na nje ya nchi. Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, alisema maonesho ya mwaka huu yana fursa nyingi kwa wafanyabiashara kuunganishwa na wenzao kutoka mataifa mbalimbali, huku zaidi wa kampuni 100 kutoka China zikionesha nia ya kufanya kazi na wafanyabiashara kutoka Tanzania.

"Hii ni jukwaa la vijana kutoka vyuo mbalimbali, hususani vya biashara. Watu wamepata fursa humu, wafanyabiashara wamepata fursa na kushirikiana na wafanyabiashara ndani na nje ya nchi," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Latifa Khamis, alisema mwaka huu maonesho hayo yamevunja rekodi ya miaka 47 iliyopita.

Alisema watembeleaji katika maonesho hayo wameongezeka kutoka 31,000 kwa maonesho yaliyopita hadi 59,000 mwaka huu.

Latifa alisema ukuaji uchumi wa jamii kupitia maonesho hayo ni mauzo ya papo kwa papo ya Sh. bilioni 3.65 ambayo wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa wamenufaika.

"Changamoto za kibiashara zilizotatuliwa katika maonesho hayo ni 396 wakati ajira za muda zilizopatikana ni 21,518.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema, "Zaidi ya nchi 28 zimeshiriki. Hii yote ni kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na serikali, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Biashara (TanTrade)," alisema.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian



Mganga wa kienyeji mkazi wa kijiji cha Sangambi, wilayani Chunya mkoani Mbeya, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi katika Mahakama ya Wilaya hiyo juzi, kabla ya kusomewa shtaka la kumbaka binti yake wa kumzaa mwenye umri wa miaka 17. **PICHA: NEBART MSOKWA**

MATOKEO KIDATO VI, UALIMU

# Udanganyifu wapungua, Hisabati bado maumivu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA la Mitihani (NECTA) limetangaza matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita mwaka huu, ufaulu ukiongezeka hadi wastani wa asilimia 90 kwa masomo yote isipokuwa somo la Hisabati ambalo ufaulu wake ni wa asilimia 78.

Hata hivyo, ufaulu wa somo la Hisabati umeongozeka kulinganishwa na mwaka jana ambao ulikuwa wa asilimia 68. Ufaulu wa jumla umeongezeka kwa asilimia 99.92.

Akitangaza matokeo hayo jana visiwani Banzibar, Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Ali Mohamed, alisema wasichana wanaongoza; waliofaulu ni 49,837 sawa na asilimia 99.61 kulinganishwa na wavulana 61,219 (asilimia 99.28).

Alisema watahiniwa wote wa shule na kujitegemea waliofanya mtihani huo walikuwa ni 111,056.

"Kwa mwaka 2023, watahiniwa waliofaulu walikuwa ni 104,549 sawa na asilimia 99.23, hivyo ufaulu wa jumla kwa mwaka huu umeongezeka kwa asilimia 0.20 kulinganishwa na mwaka 2023," alisema.

Dk. Mohamed alisema ubora wa ufaulu kwa kuzingatia madaraja kwa watahiniwa wa shule unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa 102,719 sawa na asilimia 99.4 wamepata ufaulu mzuri wa madaraja ya kwanza hadi la tatu.

Alisema watahiniwa wengi wapo katika ufaulu wa daraja la kwanza na la pili ambapo daraja la kwanza ni watahiniwa 47,862 sawa na asilimia 46.32 na daraja la pili ni 42,359 sawa na asilimia 40.99.

Katibu huyo alisema kuwa mwaka jana watahiniwa waliopata ufaulu wa madaraja ya kwanza hadi la tatu walikuwa 95,442 sawa na asilimia 99.30, hivyo ubora wa ufaulu kwa mwaka huu umeongezeka kwa asilimia 0.1 kulinganishwa na mwaka jana.

Alisema watahiniwa wa shule waliofaulu ni 103,252 sawa na asilimia 99.92 ya watahiniwa wenye matokeo, ambapo wanawake ni 46,615 sawa na asilimia 99.93 na wavulana 56,637 sawa na asilimia 99.91 na watahiniwa walioshindwa mitihani kwa sababu mbalimbali ikiwamo za kiafya ni 84 sawa na asilimia 0.08.

"Mwaka 2023 watahiniwa 96,010 sawa na asilimia 99.90 ya watahiniwa wa shule walifaulu mtihani huo, hivyo ufaulu wa watahiniwa wa shule umeongezeka kwa asilimia 0.02 kulinganishwa na mwaka jana," alisema.

Kwa upande wa watahiniwa wa kujitegemea, Dk. Muhamed alisema waliofaulu ni 7,804 sawa na asilimia 93.34 ambapo mwaka jana walikuwa 8,539 sawa na asilimia 92.30.

Alisema ufaulu wa watahiniwa hao kwa mwaka huu umeongezeka kwa asilimia 1.04.

Kuhusu ubora wa ufaulu, Dk. Mohamed alisema kwa kuzingatia madaraja waliopata watahiniwa wa shule, unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa 102,719 sawa na asilimia 99.40, wamepata ufaulu mzuri wa madaraja ya kwanza hadi tatu.

**MATOKEO YALIYOFUTWA**

Dk. Mohamed alisema baraza hilo limezuia kutoa matokeo ya watahiniwa 326 kati yao, 304 ni kidato cha sita na 12 ya ualimu.

Alisema matokeo hayo yamezuiwa kutokana na matatizo ya kiafya ambapo walipata matatizo na kushindwa kufanya mitihani na watahiniwa hao wamepewa fursa kufanya mitihani yao mwaka 2025.

Kuhusu matokeo yaliofutwa, Katibu Mtendaji huyo alisema watahiniwa 24 wakiwamo 22 wa kidato cha sita wamefutiwa matokeo yao. Kati ya hao, 17 wa shule na watano wa kujitegemea na wawili kwa ngazi ya ualimu ambao walibainika kufanya udanganyifu.

Alisema udanganyifu uliofanyika kwa watahiniwa hao ni pamoja na kuingia na simu katika chumba cha mitihani, kusaidiana kwa kupeana majibu na waliokutwa na notsi.

Dk. Mohamed alipongeza watahiniwa wote kwa kuwa na utulivu na kuzingatia taratibu za mitihani katika kipindi chote cha uendeshaji mitihani pamoja na kamati za uendeshaji mitihani za mikoa, wakuu wa shule, wasimamizi na wasahihishaji mitihani hiyo.

Alisema licha ya changamoto mbalimbali zilizojitokeza zikiwamo za mafuriko yaliyotokana na mvua na baadhi ya shule kuharibika kwa miundombinu pamoja na kimbunga Hidaya, wanafunzi walisoma kwa bidii na kufanikiwa kufaulu vizuri.

# Jafo aahidi kulinda wawekezaji nchini

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, amesema katika utawala wake hatapenda kuona Watanzania wakienda kufanya uwekezaji nchi nyingine.

Amesema Watanzania kuwekeza nje ya nchi kunaruhusu kuhamisha biashara, uchumi na ajira za Watanzania waliokuwa wanufaike.

Dk. Jafo aliyasema hayo juzi wakati akizungumza kwenye mkutano wake na viongozi wa vyama vya biashara Tanzania uliofanyika jijini Dar es Salaam.

"Sitapenda kuona Watanzania wanakwenda kuwekeza nchi nyingine, lazima tujadili hapa ni vikwazo gani vinawafanya kwenda kuwekeza kwa wenzetu na kuacha kuwekeza Tanzania na kusababisha kupoteza ajira za Watanzania waliokuwa wanufaike," alisema.

Waziri Jafo alisema uwekezaji unaofanyika nje hauna faida kwa sababu bidhaa hizo zikishazalishwa zinaletwa kuuzwa nchini.

Alisema hatapenda kuona viwanda na biashara zinafungwa bali kuendelea kuongezeka nchini.

Aliahidi serikali itaendelea kupokea na kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto zote zitakazowasilishwa na makundi hayo ili kuhakikisha Tanzania inakuwa sehemu salama ya biashara na uwekezaji.

Alisema nchini kuna fursa nyingi na maeneo mengi ya uwekezaji ambayo yanatakiwa kutumiwa na Watanzania na wageni wengine kutoka nje.

Alitaja maeneo makuu ya uwekezaji ni kilimo, madini na utalii; kuna maeneo makubwa na fursa za kutosha.

Alitaja mambo makubwa mawili ambayo ni changamoto katika sekta hiyo ni masuala ya sera na kodi ambayo kwa pamoja wanaweza kuyaboresha na kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Makamu wa Rais na Meneja Mikakati wa Airpay Tanzania, Mihayo Wilmore, alisema kwa upande wa biashara ya usafirishaji fedha kidigitali, changamoto yao ni kutotambulika kama wafanyabiashara.

Alisema changamoto nyingine ni kutakiwa kufungua kampuni yenye ofisi kwenye Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ilhali hawahitaji kuwa na ofisi ili wafanye biashara.

Alisema kutokana na vikwazo mbalimbali, soko la biashara mtandaoni limekuwa chini nchini kulinganisha na mataifa mengine.

"Biashara iliyofanyika nchini ni ya Dola za Marekani milioni tisa pekee wakati Kenya wamefanya ya Dola za Marekani milioni 240.

"Tanzania tumepakana na nchi saba na nchi zote zinahudumiwa na bandari yetu ya Dar es Saalam lakini biashara ya fedha mtandaoni tupo chini kuliko wenzetu ambao wamepakana na nchi moja tu," alisema Wilmore.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), Paul Makanza, alitaja maeneo makubwa matatu yenye matatizo katika sekta hiyo kuwa ni kodi na tozo, sheria na taratibu na uingizaji bidhaa kutoka nje ambazo nyingine zinazalishwa nchini.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabisha (JWT), Hamis Livembe, alisema hoja za wafanyabishara walishaziwasilisha na zipo kwenye maazimio ya serikali waliyatoa Juni 25 mwaka huu, hivyo wanasubiri utekelezaji wake.

# DC aamuru watoto waliofungiwa msikitini warejeshwe kwa wazazi

**Na Restuta James**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Petro Magoti, amefunga kituo kinachofundisha imani ya dini ya Kiislamu kwa watoto katika Msikiti wa Salaf ulioko Kiluvya Madukani, wilayani humo na kutoa saa 24 kurejeshwa kwa wazazi wao.

Magoti alifikia uamuzi huo wiki hii alipotembelea msikiti huo usiku akiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama, huku akitoa maelekezo kwa Sheikh Abdul Hamid kuweka mazingira sawa na kupata kibali cha kutoa elimu hiyo.

Alisema mazingira wanayolelewa hayastahili kulea watoto kutokana na ufinyu wa eneo na kutoridhishwa na hali ya usafi na usalama wa watoto.

Alisema amebaini kwamba kituoni huko, kuna watoto wenye umri kuanzia miaka mitatu ambao wamekatishwa masomo huku wengine wakitakiwa kuwa sekondari. Idadi ya watoto waliokuwa msikitini huko wakati wa ziara ya Magoti ni kutoka mikoa ya Mtwara (25), Singida (15), Morogoro (9), Pwani (2), Tunduru (1), Tabora (2), Lindi (2), Tanga (3), Iringa (5), Kigoma (2), Dar es salaam (1) na mmoja kutoka Kenya.

"Sasa unabananisha watoto kama nyanya. Tumekuja Kiluvya hapa kuna watoto 96, lengo la sheikh ni nzuri, dini yetu ni nzuri, lakini mazingira ya hawa watoto si sahihi, anaweza kutokea nyoka, mtoto akaugua malaria, akaugua kipindupindu.

"Watoto wanapangwa kama nyanya. Halafu mzazi unamleta mtoto hujui anaishi wapi? Analalaje, anakulaje," alionya.

Sheikh Hamid alisema msikiti huo ulianza kutoa mafunzo hayo mwezi Mei 2022 na wamekuwa wanapokea watoto kutoka mikoa mbalimbali.

Alisema mipango iliyopo ni kujenga mabweni ambayo tayari mhandisi ameshawapatia mchoro, huku baadhi ya malighafi za ujenzi kama kokoto na nondo zikinunuliwa.

Baada ya kutoka Masjid Aslaf, timu ya Mkuu wa Wilaya ilikwenda pia Masjid iitwayo Abdulaziz Ashlak, ambako nako ilikuta watoto wakiwa wamelala katika mazingira yasiyo rafiki na salama.



Mbunge wa Jimbo la Kiteto, mkoani Manyara, Edward Ole Lekaita (katikati) akipokewa na wakazi wa kijiji cha Makame juzi, alipowasili kwa ajili ya kuzungumza nao na kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanawake wataka masuala ya kijinsia, uwajibikaji Dira 2050

**Na Romana Mallya**

WAKATI nchi ikiwa katika maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, wanawake wamesema masuala ya kijinsia yawekwe yanapaswa kuzingatia kila sehemu.

Wamesema kuwekwe utaratibu shule zote zitoe taulo za kike bila malipo na kujengwe misingi ya uwajibikaji dhidi ya ubadhirifu wa rasilimali za taifa.

Hayo yalibainishwa juzi katika kongamano la kitaifa la wanawake kuhusu ukusanyaji maoni ya Dira ya 2050 lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wajumbe wa Tume ya Mipango na Uratibu (TDV2050) ilikuwa miongoni mwa walioshiriki.

Kongamano hilo, pamoja na mambo mengine, limelenga kujenga uelewa wa pamoja kuhusu suala hilo na mchango wake kwa maendeleo ya wanawake.

Akifungua kongamano hilo, Mwenyekiti wa TGNP, Gemma Akilimani, alitaja mambo ambayo wanatakiwa kuyatilia maanani ni pamoja na kuja na mabadiliko ya yale yaliyotiliwa mkazo kupitia mpango huo.

Alisema wanatazamia sekta zote zijikite katika mchakato utakaobainisha masuala ya kijinsia katika mpango huo, bajeti na utekelezaji wake.

"Kwa maandishi tunaweza kukuta suala la jinsia limetajwa kama kipengele tu, ukweli ni lazima masuala ya kijinsia yawekwe katika kila mchakato.

"Hii inamaanisha kwamba, kufanya uchambuzi wa kina wa masuala hayo ikiongozwa na takwimu zinazokidhi mipango na ugawaji rasilimali.

"Hakuna kinachowezekana kutekelezwa bila kuzingatia masuala ya kijinsia katika mipango ya bajeti," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya, alisema ili kuwa na mrengo huo lazima madai yao yazingatie.

"Sisi ndio tunaoandika dira na tunaamini tunayozungumza hapa yatabebwa kwa uzito wake. Ushiriki wa wanawake hata huko nyuma ni mdogo sana, tunaamini tunapozungumzia suala la wanawake tulibebe kwa uzito wake na madai tunayotaka yaweze kuingia katika dira," alisema.

Anna alitaja maoni ya wanawake watakayo ili kuingizwa katika Dira 2050, ni mchakato huo uendelee kuwa shirikishi na jumuishi, ili iwe yenye mrengo wa kijinsia.

Kuhusu maisha bora na mazuri, Anna alisema ifikapo mwaka 2050, wanadai kusiwapo kaya itakayokuwa na ukosefu wa chakula bora na cha kutosha au watoto na watu wazima wenye matatizo yatokanayo na lishe.

Anna alisema elimu inayotolewa iwe ya kumkomboa mwanamke kudai haki zake na kumwezesha kujisimamia na kutumia vipaji vyake kama raia huru.

"Jamii na mitazamo inayohalalisha ubaguzi wa kijinsia, tunataka dira inayokuja iweke elimu itakayosaidia wanawake na jamii kuzingatia masuala haya.

"Kuhakikisha shule zote zinatoa taulo za kike bure kwa sababu inasikitisha unapoona bajeti katika vitu vyenye kodi, taulo za kike zinaletewa kodi. Ni adhabu wanawake kuingia hedhi kwa mwezi?

"Kwanini ziwekewe kodi au masharti magumu? Tunahitaji taulo za kike zitolewe bure kama moja ya zana ya elimu kwa sababu ni haki," alisema.

Alisema suala la usawa wa kijinsia liingizwe katika maeneo yote ya Dira 2050 ikiwamo kwenye utangulizi, malengo, utekelezaji, ufuatiliaji wake waone sekta zote zikiwamo uchumi, uongozi, siasa, umiliki wa rasilimali na ufanyaji uamuzi kote kuwekwe.

Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Liundi, katika uchambuzi yakinifu wa Dira 2020/25, alisema Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, aliwahi kukiri kwamba dira haitakuwa na maana yoyote wala maendeleo endapo kila mtu hatawajibika kuimarisha umoja na utengamano.

"Kwetu wanamtandao tamko hili la Rais Mkapa ni msingi elekezi ambao tunatarajia uendelee kuingizwa na kusimamia masuala ya usawa wa kijinsia sehemu zote muhimu za dira, kinyume chake utaathiri utekelezaji wake," alisema.

MBAKAJI MUUAJI

# Wawili watiwa mbaroni

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawahoji watuhumiwa wawili kuhusiana na matukio ya ulawiti na ubakaji watoto kisha kuwaua yaliyotokea Mbagala na Temeke, wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam hivi karibuni.

Vilevile, jeshi hilo linamsaka mtuhumiwa anayedaiwa kujiteka wakati anatuhumiwa kuhusika na matukio ya kuteka wafanyabiashara wakubwa ili kujipatia fedha, likiwamo la Septemba 11, 2023, waliloiba Sh. milioni 357 za mfanyabiashara mwenye asili ya kihindi baada ya kumteka.

Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana, akibainisha kuwa matukio ya ubakaji watoto yalitokea kati ya mwezi Machi na Julai mwaka huu.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi linafanya jitihada kubwa kwa kushirikiana na wananchi na mamlaka nyingine za kisheria kuhakikisha watuhumiwa wengine waliohusika wanakamatwa, kuhojiwa kwa kina na kufikishwa katika mifumo ya kisheria.

"Tangu mwezi Machi mpaka Julai Jeshi la Polisi limepokea taarifa nne kutoka kwa wazazi wa Mbagala na Temeke ambapo katika matukio hayo, matatu yalisababisha vifo, lakini si kweli kwamba watoto hao walinyofolewa sehemu za viungo vya miili yao kama inavyodaiwa na baadhi ya taarifa za mitandaoni," alisema Kamanda Muliro.

Alisema Jeshi la Polisi linachunguza na linafuatilia kwa karibu taarifa inayosambaa katika mitandao ya kijamii kuhusiana na kupotea kwa mtu mmoja anayefahamika kwa jina la Adinani Mbezi (32), maarufu Adam, mkazi wa Kinyerezi.

Alisema kwa mujibu wa taarifa hiyo, inadai mtu huyo alikamatwa na polisi mkoani Mwanza na kusafirishwa hadi Dar es Salaam ambapo inadaiwa alikuwa akihamishwa katika vituo mbalimbali vya polisi Dar es Salaam, huku ndugu wakipigiwa simu na watu wanaodaiwa kuwa ni askari polisi.

Alisema wanapigiwa simu kwa namba tofauti na kuombwa watume fedha kupitia namba za simu mbalimbali ili ndugu yao aachiwe huru ambapo mpaka sasa hawajamwona na sasa simu hizo hazipatikani.

"Ukweli wa tukio hili ni kwamba, Jeshi la Polisi linamtafuta mtu huyo anayejulikana kwa jina la Adinani na wenzake kwa tuhuma za kuteka watu hasa wafanyabisahara wakubwa, huku wakati wakitenda makosa hayo walikuwa wakijitambulisha kama maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), polisi au Usalama wa Taifa.

"Watuhumiwa hao Septemba 11, 2023, walimteka mtu mmoja mwenye asili ya Kihindi aliyejulikana kwa jina la Maaz Mohamed (27), mkazi wa Upanga, saa 5:05 asubuhi maeneo ya barabara ya Bibi Titi, wakamnyang'anya Sh. milioni 357 na dola za Marekani 38,000, walimwachia baada ya kupora fedha hizo kwa sharti la baadaye kuwamalizia Sh. milioni 100, vinginevyo watapoteza maisha yake," alisema.

Kamanda Muliro alisema baada ya polisi kupata taarifa, siku iliyofuata (Septemba 12), saa nane mchana, waliwekewa mtego maeneo ya Daraja la Tanzanite walipotaka kumteka tena mfanyabiashara huyo.

Alisema watuhumiwa hao walipotaka kukamatwa walikurupuka na gari lenye namba T 146 DPY ambalo baadaye walilitelekeza eneo la Muhimbili wakakimbia.

"Gari lilivutwa na polisi na kuwekwa Kituo cha Polisi Salendar Bridge kama sehemu ya kielelezo cha tukio hilo la kumteka mfanyabiashara huyo.

"Watuhumiwa hao bado wanatafutwa na si kweli kwamba walikamatwa Mwanza na kuletwa Dar es Salaam na kuzungushwa katika vituo vinavyotajwa na taarifa hiyo iliyotolewa si ya kweli," alisema.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watendaji walioingilia zabuni na kusababisha hasara wawajibishwe

**UAMUZI** wenye utata wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuingilia zabuni yenye thamani ya Sh. bilioni 9.80 katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), umesababisha hasara ya zaidi ya Sh. milioni 700.

Hata hivyo, hadi sasa hakuna mtendaji wa serikali aliyewajibika wala kuwajibishwa kutokana na hasara hiyo.

Ni miongoni mwa hoja zilizomo katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23 ambamo anabainisha kuwa kitendo cha wizara kuingilia mchakato wa ununuzi NCAA kimesababisha ongezeko la gharama kwa Sh. milioni 702.68.

Katika ripoti yake ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka 2022/23, CAG anasema NCAA ilikuwa na zabuni Na. EA/055/2020-2021/HQ/W/01 kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka hiyo.

Ni zabuni iliyotolewa tarehe 9 Machi 2022 kwa gharama ya mkataba ya Sh. bilioni 9.80 baada ya taratibu za tathmini.

Hata hivyo, mnamo tarehe 21 Aprili 2022, zabuni hiyo ilifutwa kwa kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mdhibiti anasema kuwa, wizara tajwa ilielekeza NCAA kufuta na kutangaza upya zabuni hiyo.

Zabuni ilitangazwa tena tarehe 06 Mei 2022, na mzabuni huyohuyo aliyetangazwa mshindi awali, alipewa tena mkataba wenye thamani ya Sh. bilioni 10.48.

Hiyo ina maana kwamba, mkataba mpya ulikuwa juu zaidi kwa Sh. milioni 686.60 huku CAG akibainisha kuwapo gharama nyingine za mchakato wa pili wa zabuni Sh. milioni 16.08.

Kanuni ya 231 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 75 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2016, inaelekeza iwapo kulikuwa na malalamiko yoyote kuhusu uteuzi wa mzabuni aliyeshinda katika mchakato wa zabuni, wazabuni ambao hawakufanikiwa walitakiwa kutoa malalamiko ama kwa kuyapeleka kwa Ofisa Masuuli wakati wa muda wa kusubiri au kwa kukata rufani kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na si vinginevyo.

Hivyo, uamuzi wa wizara kuingilia zabuni ni ukiukwaji Sheria ya Ununuzi wa Umma na kutofuatwa kwa taratibu, hali iliyosababisha ongezeko la bei ya mkataba na kuchelewesha utekelezaji wa ujenzi.

Nipashe Jumapili tunaungana na CAG kwamba hapakuwa na mantiki ya kufutwa kwa zabuni hiyo awali.

Tunashauri serikali kufanya uchunguzi ili kubaini iwapo hasara hiyo ilisababishwa na uzembe au kushindwa kutekeleza majukumu ipasavyo.

Kuagiza zabuni ifutwe na kutangazwa upya kisha kutunuku zabuni hiyo kwa mzabuni yuleyule aliyeshinda awali, kuibua shaka kuhusu uadilifu wa waliotoa uamuzi huo.


Tunashauri suala hili lichunguzwe na mamlaka husika kwa kuwa kuna viashiria vya ukosefu maadili kwa waliotoa uamuzi tajwa.

Nipashe Jumapili tunatambua kwamba Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Kifungu cha 27, inamtaka CAG anapokagua hesabu za taasisi, akibaini viashiria vinavyoangukia katika makosa ya rushwa, aiarifu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili suala hilo lifanyiwe kazi hata kabla ya ripoti yake uakguzi kuwa wazi kwa umma.

Kama ilivyodokezwa awali, kufuta zabuni kisha kutunuku kwa mzabuni yuleyule aliyeshinda awali huku malipo ya mkataba yakiongezwa, kunaibuka shaka dhidi ya uadilifu wa watendaji hao wa serikali. TAKUKURU ichunguze suala hili kwa manufaa ya umma.

Ni muhimu hatua zichukuliwe ili kutoa fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo au wenye nia ya kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, hivyo kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa mali ya umma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hongera CCM kwa kubana wagombea 'mizigo', lakini...

**UCHAGUZI** wa Serikali za Mitaa umepangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu. Ni wakati ambao Watanzania watachagua viongozi watakawaongoza katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Wakati maandalizi ya uchaguzi yakiendelea, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeweka wazi msimamo wake kuhusu uchaguzi huo; kwamba safari hii hakitakuwa tayari kuweka wagombea ambao si chaguo la wananchi.

Sababu za kuja na msimamo huo zinaelezwa na Katibu wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla, kuwa ni kutokana na fundisho ambalo chama kimepata.

Makalla anasema kimebaini kuwa mgombea anayekataliwa na kisha chama kumpitisha, anakuwa si matakwa ya wananchi na anaweza kusababisha chama kushindwa katika uchaguzi.

Hatua hiyo ya CCM kuweka pembeni wagombea 'mizigo', inagusa kaulimbiu ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2019 iliyokuwa inasema; "Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa ni Chachu ya Maendeleo".

Makala anasema: "Tumeshaelezana Halmashauri Kuu za Wilaya msibebe wagombea ambao siku mnamweka tu watu wanaanza kuguna. Tunaahidi kuweka wagombea wazuri, wanaokubalika na kuwatumikia wananchi."

Kwa kauli hii, ni wazi kwamba wagombea ambao hawana uwezo wa kuongoza, maarufu 'mizigo', hawatakuwa na nafasi tena ya kuwania uongozi ndani ya chama hicho katika uchaguzi ujao.

Pamoja na hayo, ni vyema chama hicho pia kikajikita katika kudhibiti rushwa ambayo imekuwa ikidaiwa kuwapo wakati wa kampeni za kura za maoni na kusababisha wagombea wasio chaguo la wananchi kushinda.

Wakati huu ndio ambao baadhi ya wanachama huwa walalamika kuwa baadhi ya wagombea hupenyeza rupia ili kukubalika kwa wajumbe na kwa wananchi na hatimaye kuibuka washindi.

Hivyo, ili mkakati wa kuweka pembeni wagombea 'mizigo' ufanikiwe, chama hakina budi kupenyeza watu wa kunasa wale watakaopenyeza rupia kwa lengo la kutaka wapitishwe kuwania uongozi.

Miaka ya nyuma katika kura za maoni, baadhi ya wagombea ndani ya chama waliwahi kulalamikia kuwapo kadi mpya zilizokuwa zinatolewa kwa wasio wanachama ili wapige kura kumpa ushindi mgombea.

Vilevile, kulikuwapo mtindo wa kutotumia daftari lenye orodha halali ya wanachama, badala yake kila aliyekuwa anafika sehemu ya kupigia kura, aliruhusiwa mradi ana kadi ya chama.

Vilevile, baadhi ya viongozi wa chama wamekuwa wakituhumiwa kujihusisha na mchazo huo. Hivyo, wakati huu ambao CCM inakuja na mbinu mpya, ingeziba mianya hiyo ili lengo la kupata wagombea sahihi litimie.

Kwa mfano, mwaka 2022, CCM ilisimamisha uchaguzi katika mikoa mitatu kwa nafasi zilizoonesha kuwa na changamoto na kufuta uchaguzi wa Umoja wa Vijana wa CCM (UCCM) kutokana na tuhuma za rushwa.

Hatua zilizochukuliwa na chama kipindi hicho kufuta uchaguzi, zinaonesha kuwa wagombea wasio na sifa huwa wanatumia njia isiyo halali kupata nafasi, hivyo CCM haina budi kujipanga zaidi kudhibiti kadhia hiyo.

CCM pia inapaswa kujipanga kufuatilia kwa karibu nyendo za watiania, wajumbe na wanachama, ili kujiridhisha kama hakuna harufu ya rushwa ili hatimaye wapatikane wagombea ambao ni chaguo la wananchi.

Kuna wanachama wanaamini wanapomchagua mtu katika nafasi ya uongozi, anakwenda kula, hivyo wanaona ni bora nao wapate kitu kutoka kwa mgombea kuliko kumpa kura tu. Dhana hii inahitaji elimu ya kukabiliana na rushwa kwa kuwa jinai hiyo ni hatari kwa maendeleo ya taifa.

Hongera CCM kutangaza kubana wagombea 'mizigo', lakini ni vyema mkapenya kila kona kubaini wapigakura wa aina hiyo na wagombea wao, ili lengo la kupata viongozi wanaokubalika kwa wananchi litimie.

HABARI KITAIFA

# Wanandoa jela miaka 30 kwa usafirishaji dawa za kulevya

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewahukumu Halima Maneno (39) na mume wake, Mwichande Said (50) kwenda jela miaka 30, baada ya kupatikana na hatia ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin Hydrochloride gramu 11.21.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Ushindi Swalo wa mahakama hiyo baada ya kupitia ushahidi wa vielelezo na ushahidi uliotolewa na pande zote mbili.

Hakimu Swalo alisema sheria inautaka upande wa mashtaka kuthibitisha mashtaka dhidi ya washtakiwa kwa sababu wao ndiyo wenye kesi.

Alisema kuwa ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka umethibitisha mashtaka bila kuacha shaka yoyote.

"Washtakiwa mahakama imewatia hatiani kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya kinyume cha sheria, haya upande wa mashtaka mna chochote cha kuzungumza kabla sijatoa adhabu?" aliuliza Hakimu Swalo.

Wakili wa Serikali Asiath Mzamiru alidai hawana rekodi za washtakiwa na ni wakosaji wa mara ya kwanza, hivyo wanaomba mahakama itoe adhabu kali kulingana na sheria inavyotaka.

Baada ya Wakili Mzamiru kudai hivyo, Hakimu Swalo aliwapa nafasi washtakiwa ya kuzungumza kama wana lolote la kujitetea kupunguziwa adhabu.

Wanandoa hao waliomba mahakama iwapunguzie adhabu kwa kuwa wana familia inayowategemea na pia wote ni wagonjwa wa kisukari.

"Nimesikiliza shufaa za pande zote mbili na kwa kuzingatia kuwa washtakiwa ni wakosaji wa mara kwanza, adhabu yetu kila mmoja atatumikia kifungo cha miaka 30 jela," alisema Hakimu Swalo.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi wanane na vielelezo 10 na washtakiwa hao ambao ni wakazi wa Magomeni Mwembechai, mkoani Dar es Salaam walijitetea wenyewe wakiongozwa na wakili wao.

Inadaiwa kuwa Machi 31, 2023, washtakiwa wakiwa Magomeni Mwembechai, ndani ya Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin Hydrochloride gramu 11.21.

## STAMICO yataka bei rafiki mitambo wachimbaji wadogo

Na Halfani Chusi

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk. Venance Mwasse amewataka wazalishaji mitambo ya kunyanyulia vitu vizito na uchimbaji madini, kuzalisha itakayopatikana kwa bei rahisi na kuwafaa wachimbaji wadogo.

Amesema wachimbaji wadogo wanapata shida kwa kuwa vifaa vingi vinavyoletwa nchini vimelenga zaidi wachimbaji wakubwa, jambo linalowanyima fursa wachimbaji wadogo kuvipata.

Dk. Mwese aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam alipozindua mashine ya kubebea vitu vizito na itakayosaidia katika uchimbaji madini.

Mashine hiyo imeletwa nchini na kampuni inayojihusisha na uzalishaji vifaa vya ujenzi na uchimbaji wa madini ya Meta Africa.

Katikan uzinduzi huo alisema ujio wa kifaa hicho nchini utasaidia kuongeza ajira kwa vijana na Pato la Taifa kwa ujumla.

"Mmefanya uamuzi huu mzuri kwa sababu dunia inakwenda katika nishati safi ambayo inategemea madini, lakini pia ipo katika mapinduzi ya nne ya mageuzi ya viwanda.

"Pia ni wakati ambao tunaangalia namna ya kuongeza uzalishaji katika sekta ya madini, itasaidia kutekeleza hayo, pia ujenzi wa viwanja vitakavyotumika katika mashindano ya AFCON 2027.

"Ninachoweza kusema wameleta bidhaa katika muda sahihi na soko sahihi, niwapongeze sana kwa kutuletea mitambo hiyo, wamekuja kwenye nchi ambayo inajali wawekezaji na inajali wachimbaji madini," alisema

Aliahidi STAMICHO itaendelea kutoa ushirikiano na kuwa daraja kwa wote wanaoleta vifaa vinavyoweza kurahisisha uchimbaji madini.

Mkurugenzi Mkuu wa Meta Africa, Ardish Trived alisema watakaotumia mitambo hiyo, itawasaidia kufanya kazi kwa ufanisi na kwa muda mwafaka.



Mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa (GEF), Nyamizi Mhoja akizungumza katika kikao cha kuhitimisha ziara ya ufuatiliaji wa programu hiyo kwenye taasisi za fedha, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wajasiriamali kupatiwa ripoti za utafiti wa CBE

Na Maulid Mmbaga

MKUU wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Tandi Luoga amesema wameanzisha mkakati wa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wajasiriamali na wafanyabiashara pamoja na kuwapatia matokeo ya utafiti wao ili wautumie katika kuboresha biashara.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataisa (Sabasaba), Prof. Tandi alisema kuwa mwezi Novemba kila mwaka, wamekuwa wanafanya kongamano la kimataifa linalohusisha wafanyabiashara kwa lengo la kuonesha utafiti waliofanya na unaleta matokeo katika jamii.

Alisema wamekuwa wanatumia fursa tofauti kwa ajili ya kuwafikia wajasiriamali ili kuwaongezea uelewa wa kusimamia na kukuza biashara zao ziwaletee mafanikio.

"Mwaka huu tumeanza midahalo ya wazi ambayo inashirikisha wataalamu mbalimbali kutoka ndani na nje ya chuo ambao wamekuwa wanaelimisha wajasiriamali na jamii kwa ujumla.

"Tunatumia njia tofauti ikiwamo mitandao ya kijamii ili kuwafikia Watanzania wengi," alisema Prof. Tandi.

Alisema kuwa wamekuwa wanahakikisha elimu wanayotoa inafika kwa watu wa kawaida katika sehemu tofauti ndani na nje ya Tanzania.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Nasibu Mramba, alisema wameanzisha mitaala ambayo mwanafunzi katika masomo yake ya miaka mitatu, nusu yake atakaa darasani na iliyobaki atakwenda kufanya mafunzo kwa vitendo ili kumwandaa kushindana katika soko la ajira kimataifa.

"Hii inafanya wanafunzi wetu wakidhi vigezo katika soko la ajira ambalo watu wengi wanashindwa kufanya kwa vitendo yale waliyosoma darasani.

"Kwa kufanya hivyo inasaidia watu wetu waajirike ndani na nje ya nchi na kupunguza idadi ya wasiokuwa na ajira nchini," alisema Dk. Mramba.

Alisema kuwa wanafunzi wao ambao wanaonesha nia ya kufanya kwa mafunzo kwa vitendo yale wanayosoma darasani, huwasaidia mtaji mdogo wa kuanzia ili kufanikisha malengo yao.

Alisema wamekuwa wakiunganisha wanafunzi hao na wajasiriamali wabunifu wa ndani na nje ya nchi ili waliyosoma kwa vitendo wayatekeleze kwa ufanisi zaidi.

Pia alisema huwaunganisha na taasisi za kifedha na kuwapa elimu watu ambao wanawalea ili waweze kutimiza ndoto walizonazo, kujipatia kipato na kusaidia ubunifu wao kuleta suluhu kwa Watanzania.

"Tayari tumeshawasaidia zaidi ya wanafunzi 280. Kati yao, baadhi tunao na wengine wameshamaliza chuo, wako mtaani wanafanya biashara zao, na tunaendelea kila mwaka kuingiza wapya katika mradi huu," alisema Dk. Mramba.

# HABARI KATIKA PICHA



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (wa pili kulia), akikabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Alhamishi Hazali katika Shule ya Sekondari Mwahu, kijiji cha Gehandu juzi, ambapo utakagua miradi tisa yenye thamani ya Sh. bilioni 12.4. **PICHA: GIFT THADEY**



Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini na Mbunge mstaafu wa Jimbo la Muheza mkoani Tanga, Balozi Adadi Rajabu (katikati), akizungumza wakati akitoa salamu za pole alipohani msiba wa Mwenyekiti mstaafu wa Mamlaka ya Mji wa Muheza marehemu Mashaka Mtali, katika Mtaa wa Masimbani hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Mkewe Mama Mbonimpaye Mpango wakishiriki ibada ya asubuhi katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Mshindaji, Jimbo Kuu Katoliki Kigoma jana. **PICHA: OMR**



Wachuuzi wa miwa, wakichagua bidhaa hiyo kwenye soko la Mawasiliano, jijini Dar es Salaam jana. . **PICHA: MIRAJI MSAL**A



Gari likishusha udongo kwenye eneo lenye bonde Kimara Mwisho, Dar es Salaam juzi, ikiwa ni mwendelezo wa upanuzi wa Barabara ya Morogoro ulioanzia eneo la Ubungo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# MAISHA

JULAI 14, 2024
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 13

**Vijana kazi kwenu**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Acha kuokoteza ramani ya nyumba



Ukurasa 12

**HARUSI**





# Mwili usio na mba

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| O | | K | I | L | W | A |
| N | | | | O | | N |
| E | | B | A | A | | G |
| S | A | A | | N | O | A |
| H | | N | I | A | | L |
| E | | D | | | | I |
| A | M | A | N | A | | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

BEE, NOA, GOA, YAI, PEMBA, ATOKE, BANDO, MBEYA, SINGIDA, ATWISHE

## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI





## AMSHA AKILI

 elapp ________


 eoragn ________

 gmoan ________

 lmeon ________




## CHEKA



### Alichokifanya daktari

MTOTO John alikwenda sokoni kununua samaki ambaye alitumwa na mama yake.

Alipofika alimkuta mchuuzi akiuza samaki aina ya kambale juu ya meza yake ya mbao.

**John.** Nataka samaki mkavu anauzwa bei gani?

**Mchuuzi:** Shilingi 1000 na 5000

**John:** Mi nataka aliyenyooka na sio huyu aliyejikunja

**Mchuuzi:** Hawa wamekunjwa baada ya kuvuliwa, hakuna wengine.

**John:** Kama hivyo punguza bei kwani urefu wake umepungua

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mafao yanapotenganisha wanandoa!

***KARIBU msomaji wangu tuendelee kudadavua vituko ndani ya ndoa zetu. Kila ndoa unayoiona ina changamoto zake. Na kila tikisiko kwenye ndoa lina chimbuko au chanzo chake. Hakuna kinachotokea kwa bahati mbaya.***

Nikasema maisha ni mchakato, pia mapambano. Na kwamba mwanadamu kubadilisha mawazo ni jambo la dakika kama si sekunde.

Wakati mwingine mazingira aliyoko yanaweza kumbadili mawazo au fikra fulani au kufuatilia mbali mipango fulani na kuamua vinginevyo. Yapo mambo mengi yanayochangia hali hiyo kutokea.

Leo msomaji wangu nikupe mfano wa ndoa ambayo baba na mama wote wamestaafu kipindi kimoja, ili uone jinsi maisha yao yalivyo hivi sasa. Utadhani ni ndoto, kumbe tatizo hili linazitafuna familia nyingi, lakini zinagumia maumivu kwa kujikaza kuficha aibu.

Wiki hii nikiwa kwenye tawi moja la benki nikisubiri huduma, alikuja baba mmoja mtu mzima akaketi kiti kilichokuwa wazi. Kushoto kwake aliketi dada mmoja na kulia nilikuwa mimi.

Kabla ya kuketi akitokea nyuma yetu alidondosha koti lake ili kushika ile nafasi. Kwa kuwa alijua kwa nyuma alipodondosha lile koti mimi na yule dada tulishtuka. Alipozunguka na kulichukua lile koti na kukaa, ndipo akamwambia yule dada kushoto kwake, 'usiogope'.

**"Majadiliano yakaanzia hapo. Akauliza swali moja zito, ni kwa nini wanaume hufa mapema kuliko wanawake? Hili lina mjadala mpana nitawasilisha mada yake siku za usoni.**

Alipogeuka akanikuta na mimi nimeduwaa akanisemesha nikamsalimia. Kwa ufupi, nilipomsoma ni kama alikuwa na haraka huko alikotoka na muda wa benki ulikaribia kuisha, milango ifungwe.

Akatoa namba yake ya kuitwa kwa huduma akaniuliza itaitwa wakati gani nikamwelewesha. Akanitazama akaniuliza inaonekana ni mstaafu kama mimi, nikamjibu 'ndio'. Akaniuliza mume wako yupo wapi, nikasema alishatangulia mbele za haki.

Majadiliano yakaanzia hapo. Akauliza swali moja zito, ni kwa nini wanaume hufa mapema kuliko wanawake? Hili lina mjadala mpana nitawasilisha mada yake siku za usoni.

Nikanyofoa kipengele kimojawapo kutoka hiyo mada nikamwambia, mke wako anaweza kuchangia wewe kufa mapema kama hukuweka tahadhari za kutosha.

Nilipotaja hilo ndipo baba huyo mwenye umri wa miaka 75 kama alivyotaja mwenyewe, akafunguka kuhusu vituko anavyofanyiwa na mke wake.

Akasema: Mimi ni mstaafu tangu mwaka 2018. Kipindi hichohicho mke wangu naye alistaafu na wote tulikuwa walimu.

Mimi na mke wangu tuliishi kwa raha na tulishirikiana katika mambo mengi kimaisha na tulibarikiwa kuwa na watoto na sasa tunao wajukuu kadhaa.

Cha ajabu mimi na mke wangu tumekuja kutofautiana mara tu baada ya kustaafu. Huko nyuma tulikubaliana kila mmoja akipata mshahara tunashirikishana nini cha kufanya kwa maendeleo ya familia yetu.

Lakini, baada ya kustaafu tu, mke wangu akanificha wala hakuniambia kiasi cha mafao ya uzeeni alichopata wala pensheni yake kwa mwezi ni kiasi gani. Alificha karatasi zote kuhusu mafao.

Ilibidi nidadisi kwa rafiki zake wa karibu nikagundua alipata takribani Sh. milioni 120. Lakini hakuwahi kunidokeza tangu 2018. Na pensheni yake kwa mwezi ni karibu Sh. 500,000.

Inavyoonekana wapo marafiki waliomshauri kuwa asiniambie kuhusu alichokipata, kama ni matumizi mimi nitatoa hizo za kwangu za kustaafu.

Ninamshukuru Mungu fedha zangu za kustaafu nilinunua viwanja na kujenga. Ninazo nyumba tatu ninapangisha na mkoani aliko mke wangu nyumba nilijenga mimi. Yeye alichofanya alipostaafu ni kukarabati kidogo nyumba hiyo iwe na mwonekano mzuri. Hakuna kingine hadi leo.

Hivi karibuni niliona stakabadhi ya benki yenye balansi kwenye akaunti yake Sh. milioni 30. Nikajiuliza kama alipata zaidi ya Sh. milioni 100, zingine alifanyia nini? Na kwanini hakutaka kunishirikisha kuhusu mafao yake kama tulivyokubaliana tangu awali?

Kingine hivi sasa amekuwa mtu wa hasira, jambo ambalo linanishangaza. Kwa sasa muda mwingi nipo Dar ninaandika vitabu vya shule na kazi zingine za kitaaluma katika sekta ya elimu ili maisha yangu yasonge mbele.

Ndipo nikamwambia, hiyo tafrani anayopitia katika ndoa yake ni moja ya mambo yanayochangia mwanamume kufa mapema. Anashangaa nini kimempata mkewe na pia ndani yake anaumia kwani anadai alimpenda sana.

Nilimtia moyo, kwamba "wewe ni mwanamume, lazima uhimili magumu, usitunze vitu rohoni". Pia nikamshauri ajitahidi kujipa utulivu, ale vizuri, amwombee mkewe Mungu arejeshe ufahamu wake.

***Je, una ushauri, kisa cha kimaisha? Ujumbe 0715268581. Namba hii ipo WhatsApp. Email: fwingia@gmail.com***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Tubishane kwenye siasa za ulinganisho

SIASA za ulinganisho (comparative politics) ndio aina ya siasa inayofikirisha zaidi na kuvuta hisia za wengi.

Linganisha masuala ya uchumi, kuongezeka kwa makali ya gharama za maisha, mahitaji ya ajira, kipato duni au kupaa kwa bei za bidhaa mbalimbali kunakotokana na mfumuko wa bei, utaziona sura tofauti za Watanzania.

Ulinganisho wa kushughulikia vitu badala ya watu ndio ajenda kubwa inayohusu siasa za ulinganisho.

Watanzania wanaokaa katikati ya nchi huenda wasielewe masuala ya utawala tofauti na watu wa pembezoni.

Kwa mfano, uchumi mkubwa wa Kilimanjaro unategemea kitu kinachoitwa kwa Kiingereza 'remittance'.

Ni fedha wanazotegemea wakazi wa Kilimanjaro kutumwa na watoto au ndugu walioko mbali na Kilimanjaro.

Ninatamani wanasiasa wetu wakosoane kwa hoja za siasa za ulinganisho ili kuja na mwarobaini wa matatizo ya wananchi.

Mathalani, wanaweza kukosoana ili kutafuta suluhu ya muda mrefu ya vijana wengi kupoteza matumaini ya maisha.

Vijana wengi wanakata tamaa kwa sababu hakuna kazi, wakiamka asubuhi hakuna kiwanda wanachokwenda kufanya kazi.

Matokeo yake tunayoyashuhudia leo, ni namna wanavyojipongeza kwa pombe kali na hatarishi kwa afya zao, ili tu kupunguza msongo wa mawazo.

Katika siku za usoni, nimeguswa na aina ya siasa za ulinganisho zinazofanywa na baadhi ya wanasiasa nchini.

Nimemwona mwanasiasa na mkosoaji wa serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Godbless Lema, akifanya ulinganisho wa vitu au bidhaa.

Huko katika mikutano yao inayoendelea katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, anasema Watanzania wananunua maziwa kila mwaka kwa Sh. bilioni 34.5 wanazozilipa nje ya nchi.

Anahoji, "ninyi (wananchi) mkipewa ng'ombe wanaozalisha maziwa kwa wingi, mkatengenezewa mashamba ya kuzalisha vyakula vya ng'ombe, hamwezi kufunga ng'ombe nyie?

"Mahindi pamoja na wakulima wa Tanzania kulima, serikali wanaleta kutoka nje ya Sh. bilioni 64, sukari Sh. bilioni 265, mchele tunanua kila mwaka Sh. bilioni 146, maharage ya soya Sh. bilioni 34, Sh. njano bilioni 554 na mafuta ya kula Sh. bilioni 694.Jumla yake karibu Sh. trilioni mbili.

"Vyakula vyote hivi, bidhaa zote hizi, zinaweza kulimwa Mkoa wa Manyara peke yake. Yaani maana yake, Sh. trilioni mbili ingebaki Manyara kila mwaka kwenye mazao huku tusingeona lami za kubabaisha, kungekuwa na lami, kungekuwa na vyuo, watoto wangesoma na watu wangekuwa na maisha bora.

"Uchumi ni maarifa, ndio sababu Abu Dhabi (Makao Makuu ya Falme za Kiarabu-UAE), ni jangwa lakini wana uchumi mzuri kuliko Tanzania.

"Hanang' kuna shamba la ngano, yale mashamba yamekufa. Leo tunaagiza ngano ya Sh. bilioni 500 Ukraine."

Lema anakwenda mbali zaidi akisema, "Jiulize Sh. bilioni 500 zingekuwa zinabaki Hanang' kila mwaka, Hanang' ingekuwa kubwa kuliko Dar es Salaam.

"Kahawa imesomesha vijana wote wa kichaga. Kahawa imesomesha vijana wote wa Kagera, kahawa ni zao la pili duniani baada ya mafuta kwa kuuzika.

"Kahawa leo imekufa Kilimanjaro, kahawa imekufa Kagera, kahawa imekufa kila mahali. Hata yale mazao yanayoota bila mbolea nchi hii imeshindwa kuyasimamia."

Tukosoane kwa hoja, tufanye siasa za ulinganisho, si kueleza nasaba ya mtu.

Hakuna jambo litakaloijenga nchi yetu kama kukubaliana kutokubaliana katika hoja.

Tuvumiliane, tukosoane kwa staha katika siasa za ulinganisho maana tunajenga nyumba moja.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI





Ni furaha iliyofikia kilele kwa Grace Mponeja baada ya kufanyiwa sherehe ya aina yake ya kumuaga, kabla ya kufunga ndoa takatifu jijini Mwanza hivi karibuni.





MITINDO

# Vijana kazi kwenu

MITINDO ya mavazi ni sanaa inayowapa joto vijana wa kisasa kutokana na kila kukicha kunaibuka aina mpya ya mavazi.

Licha ya idadi kubwa ya vijana kuhamasika na kuchangamkia sekta hii mpya ambayo imeanza kuwa sehemu ya kuwapatia ajira.


Katika tasnia ya sanaa ya mitindo kundi hilo linatumia njia mbalimbali ya kujipatia pesa hasa kwa kutangaza biashara za mavazi kupitia mitandao ya kijamii.

Mwanamitindo maarufu nchini, Mustafa Hassanari, amesema kwa sasa biashara ya mavazi imehamia kwenye mitandao ya kijamii na wateja wengi ni vijana.


Alisema wao kama wabunifu wanafurahia kupanuka kwa wigo wa mitindo, hasa kwa kuzingatia mahitaji ya soko linalofanyika kidijitali.

Amesema kinachotakiwa kwa sasa wabunifu wa ndani kuelewa nini wanatakiwa kufanya ili kukidhi mahitaji ya soko la sasa ambalo linahitaji ubora, umakini na kwenda na muda.

"Kama wabunifu tunataka kuionyesha dunia kwamba tanzania tuna vipaji vya ubunifu ambavyo vinakidhi na hali ya mahitaji kuliko huko nyuma," "amesema wao wanashindwa kuzithamini, ni vema wakabadilika sasa, ukiangalia wasichana au wakina mama wanaotumia bidhaa za ndani wanazielewa wanapendeza sana na ni wa tofauti."









UREMBO





# Mwili usio na mba


TATIZO la mba kwenye ngozi ni miongoni mwa mambo yanayosababisha mtu kukosa muonekano mzuri na wakati mwingine kukumbana na unyanyapaa katika jamii.

Kitaalamu mba ni aina mojawapo ya magonjwa yanayotokana na fangasi yanayoambukizwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

Wanawake wengi wanakumbana na matatizo haya ya mba, kutokana na kupaka aina ya vipodozi vinavyowaletea athari katika ngozi zao.

Unapokumbana na tatizo la namna hii ni vizuri kujipaka dawa zinazofaa badala ya kutafuta krimu ambazo ni hatari zaidi.

Mbegu za papai ni tiba nzuri ya asili ambayo haiwezi kukuletea madhara zaidi.



**Jinsi ya kuondoa**

Mbegu za papai ni dawa ya asili inayoweza kutibu ngozi yako na kukuondolea tatizo la kuwashwa au mabaka yanayokukabili.

**Namna ya kutumia**

Unachotakiwa kufanya ni kuchukua mbegu za papai na kuziponda kwa kutumia kinu au Brenda.

Kisha anza kujipaka sehemu ambako kuna mabakabaka ya mba huo.

Unaweza kurudia kila mara hasa wakati wa kulala hadi utakapoona mba huo unaondoka na kuwa na ngozi nyororo badala ya kutumia vipodozi vikali.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Ndizi mbivu kwa nazi

WENGI tumezoea kupika ndizi mbichi aina ya mshale, mzuzu au bukoba lakini leo tunaelekezana kupika ndizi mbivu.

**Mahitaji**

Ndizi mbivu za kupika 10 aina ya mzuzu, nazi kavu tatu, sukari kiasi na hiliki kiasi.



Menya ndizi zako kwa kuzipasua katikati kwa marefu,



uziondoe taratibu ndani ya ganda lake.



Zimenye kisha maganda uyaoshe. Yapange vizuri maganda hayo ndani ya sufuria safi (kwa chini). Chukua vipande vya ndizi uvipange juu ya maganda.

Kuna nazi uchuje tui zito utenge na jepesi utenge. Chukua tui jepesi ulitie katika ndizi kisha uziache. Zipike mpaka tui likauke na ndizi ziive. Nyunyuzia sukari kidogo. Twanga hiliki utie juu yake.

Chukua lile tui zito ulimimine uache liwe linatokota kwa moto mdogo sana. Tui likiauka na kutoa mafuta epua na uziache zipoe. Unapopakua, zitoe taratibu bila ya kuzivuruga.

MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

## Tupia kikabati cha glasi sebuleni

KUIPAMBA nyumba ni jambo lisiloisha na lisilopitwa na wakati. Kila wakati nyumba inahitaji mabadiliko ya kupunguza vitu au kuongeza kutokana na kile ambacho mwenye nyumba anataka kukiona.

Mtaalamu wa mapambo ya nyumba, Deogratius Thomas, anaeleza kuwa kikabati cha 'glasi tupu' sebuleni ni pambo lisilo kifani.

Anasema pamoja na kwamba nia ni kupamba, glasi hizo zinaweza kuwekwa mahsusi kwa ajili ya mvinyo au pombe kali.

Kwa wasiotumia kilevi, anasema glasi hizo zinaweza kutumika kumhudumia mgeni au mwenyeji kinywaji akipendacho akijichagulia kutokea eneo hilo.

"Kwenye hiki kikabati unaweza kuweka jagi za barafu (ice cubes) za ukubwa tofauti ili ukipata wageni wachache uweze kuwahudumia kwa size ya kijagi...unaweza kuweka mshumaa ambao ukiamua unaweza tu kuuwasha mara moja moja," anasema.

Deo anasema kabati hilo linapaswa kuendana na ukubwa wa eneo akishauri kuwa kwa nyumba yenye nafasi kubwa, kabati liwe kubwa na kwa nyumba ndogo liwe dogo.

"Ni muhimu sana kumtafuta fundi akushauri maana unaweza kuona picha mtandaoni, ukaenda kuchongesha kamati ukija kuliweka ndani halikai vizuri kwa hiyo ni muhimu fundi akapima na kutoa ushauri kulingana na chaguo la mteja," anasema.

Anasema baadhi ya watu wanaweka glasi, midoli na picha moja kwenye kabati hilo ili kunogesha.

Anashauri pia kwamba, kwa kuwa linafaa kuwekwa vinywaji vichache, ni muhimu kuweka 'opener' eneo hilo.

Zingatia: Siyo lazima liwekwe sebuleni. Linaweza kuwekwa kwenye kona au eneo la chakula.





# Acha kuokoteza ramani ya nyumba

UJENZI wa nyumba hauwezi kufanyika pasi na ramani inayoonesha dira ya aina ya nyumba inayotakiwa kujengwa.

Pamoja na kutakiwa kuwapo ramani kabla ujenzi wa nyumba, wapo baadhi ambao wamekuwa hawalichukulii kwa umakini suala la kuwa na ramani kutoka kwa wataalamu wanaoeleweka na badala yake 'kuokoteza' tu.

Mtaalamu wa masuala ya ujenzi, Lameck Kashabo, anasema kuokoteza ramani na kutokuthamini kile unachokwenda kujenga licha ya kwamba unatumia mamilioni ya shilingi kujenga ni hatari na mwisho wake huwa majuto.

"Inashangaza sana kwamba unakuta mtu anakwenda kujenga nyumba ya Sh. milioni 90 lakini anaokoteza ramani kutoka kwa wasio wataalamu au anatafuta ramani ambayo imetumiwa na mtu mwingine wakati gharama ya kumtumia mtaalamu kwa huduma yote ya ushauri pamoja na michoro labda ni Sh. 600,000 ambayo haifiki hata asilimia moja ya gharama yote ya ujenzi. Uamuzi wa aina hii kwa vyovyote vile unaambatana na hasara kubwa na majuto ya baadaye," "Madhara ya kuokoteza ramani ya nyumba kisha ukaijenga, iwe ni kutoka kwenye mitandao au ni kutoka kwa mafundi wa mitaani au kwa namna nyingine yoyote ile ni kushindwa kuthamini nyumba unayotaka kujenga licha ya kwamba unakwenda kutumia fedha nyingi sana kuijenga," anaonya Kashabo.






Anasema miongoni mwa madhara ya kuokoteza ramani ni kushindwa kupata aina ya nyumba unayotaka kwa kulazimika kukubaliana na chochote unachokutana nacho kwenye ramani unayookoteza.

"Kila mtu huwa na vipaumbele tofauti na vya mwingine, karibu kila kazi tunayokutana nayo huwa ni vigumu kufanana na ya mtu mwingine kwa vipaumbele vya kimahitaji, achilia mbali utofauti wa ukubwa wa viwanja, utamaduni na mengineyo, na ndiyo maana huwa ninawashauri watu kufanya kitu kinachoendana na vipaumbele vyao.

"Huwezi kufurahia nyumba ambayo si chaguo lako, hata kama ikitokea ukapenda aina fulani ya jengo au nyumba kutokana na muundo wake, bado kwa ndani kuna vitu hutavifurahia namna jinsi vilivyopangika hivyo unachotakiwa ni kuchukua picha ya lile jengo ulilolipenda na kisha kumwonyesha mtaalamu, kumwambia kwamba 'ninataka liwe na mwonekano huu' lakini ukamwelekeza alipangilie upya kwa ndani na mwisho wa siku libaki na mwonekano ule unaoupenda wewe.

"Unaweza kujuta sana baadaye unapookoteza ramani, kisha ikajengwa kama ilivyo au hata kama itabadilishwa ikawa kienyeji sana na hata usiipende tena. Bila kutumia utaalamu sahihi mara nyingi changamoto zake unakuja kukutana nazo baada ya kuanza kuitumia," anasema mtaalamu huyo.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO. ...JAPO DUNIA NI TAMBARA BOVU, LAKINI HUWEZI KUPIGIA DEKI...

## HABARI KIMATAIFA

# Rais mpya Iran akubali mazungumzo na Ulaya

**TEHRAN,** IRAN

RAIS wa Iran, Massoud Pezeshkian, ametangaza kuwa yuko tayari kushiriki mazungumzo yenye kujenga na nchi za Ulaya.

Akizungumza hivi karibuni, kiongozi huyo aliyeingia madarakani wiki mbili zilizopita amesema nafasi iko wazi kuanza mazungumzo hayo ambayo yatanufaisha pande zote mbili.

Rais Pezeshkian alitoa tangazo hilo na makala yake ilichapishwa jana katika Gazeti la kila siku linalozungumza Kiingereza.

Hata hivyo aliwakosoa kwa kurejelea ahadi zao walizozitoa kuhusu suala la nyuklia.

Pezeshkian, mwenye miaka 69, aliyechaguliwa katika duru ya pili ya uchaguzi wa urais mwanzoni mwa mwezi Julai, ataapishwa mwishoni mwa mwezi huu ili kuanza muhula wa miaka minne.

Uchaguzi wa urais ulifanyika Julai 5, ulifuatiliwa kwa karibu na mataifa ya nje, wakati nchi hiyo inakabiliwa na migogoro kadhaa ya kijiografia, kuanzia vita vya Gaza hadi suala la nyuklia.

Wakati wa kampeni zake za uchaguzi, Pezeshkian aliahidi kuitoa Iran katika shimo baada ya kutengwa na nchi kadhaa zenye nguvu kwa kuanzisha mahusiano ya kujenga na hasa nchi za Ulaya.

Wakati wa kampeni, Massoud Pezeshkian aliahidi kufanya mazungumzo na serikali ya Marekani ili kuanzisha upya mazungumzo kuhusu nishati ya nyuklia ya Iran na kuondoa vikwazo.

**RFI**



Waokoaji wakijaribu kuokoa watu walionusurika kwa kusaidiana na raia baada ya jengo la shule kuporomoka katika mji wa Jos, jimbo la Plateau nchini Nigeria, jana. **PICHA: AP**

## Polisi Kenya kuchunguza maiti zilizofungwa kwenye viroba

**NAIROBI,** KENYA

JESHI la polisi nchini Kenya, limesema linachunguza tukio la maiti zilizokatwakatwa na kufungwa kwenye viroba na kisha kutupwa kwenye dampo la takataka jijini Nairobi.

Taarifa kutoka Idara ya polisi nchini humo, zilieleza uchunguzi unalenga kubaini kama askari wake wanahusika na tukio hilo au watu wengine,

Jumla ya maiti 10 zilipatikana juzi zikiwa zimetupwa katika dampo hilo lililoko eneo la Mukuru, ambalo linakaliwa na watu maskini katika jiji hilo.

Idadi hiyo inaweza kuongezeka kutokana na juhudi ya kutafuta miili mingine zilikatizwa baada ya watu wengi kukusanyika eneo hilo na ilibidi kutawanywa na mabomu ya machozi.

Wiki mbili zilizopita vijana wanaojiita Gen Z, waliitisha maandamano kupinga muswada wa fedha ambayo yalivunjwa na polisi ambao walitumia nguvu ya ziada.

Kutokana na maandamano hayo, Mkuu wa polisi nchini humo, Inspekta Jenerali Japhet Koome alitangaza kujiuzulu.

Tukio hilo la kupatikana kwa miili hiyo katika mifuko ya plastiki, linarudisha kumbukumbu mbaya katika Mto Yala baada ya maiti 40 kupatikana zikiwa katika hali hiyo.

Mashirika ya haki za binadamu yameshuku kuwa miili hiyo ni ya wahanga waliouawa wakiwa mikononi mwa vyombo vya dola.

Mamlaka Huru ya Kusimamia Polisi (IPOA) pia inachunguza madai ya utekaji nyara na kukamatwa kinyume cha sheria kwa waandamanaji ambao walitoweka kufuatia maandamano yaliyoenea dhidi ya serikali.

**RFI**

## Wauaji mgombea Ecuador wahukumiwa miaka 34 jela

**QUITO,** ECUADOR

WATU watano wanaohusishwa na genge la kihalifu nchini Ecuador, wamehukumiwa kifungo cha miaka 34 jela baada ya kupatikana na hatia ya mauaji ya mgombea urais, Fernando Villavicencio, mwaka jana.

Villavicencio, ambaye alikuwa m bunge na mwanahabari wa zamani, aliuawa kwa kupigwa risasi wakati alipokuwa akitoka kwenye mkutano wa kampeni katika mji mkuu, Quito, Agosti mwaka jana.

Carlos Angulo, anayedaiwa kuwa kiongozi wa genge la Los Lobos, na Laura Castilla walihukumiwa kifungo cha miaka 34 na miezi minane jela kwa kuongoza mauaji hayo.

Watuhumiwa wengine ambao wanaume wawili na mwanamke mmoja walihukumiwa kifungo cha miaka 12 kwa kusaidia genge lililofanya shambulizi hilo.

Waendesha mashtaka walidai kuwa Angulo - anayejulikana sana kama The Invisible, aliongoza shambulizi hilo kutoka katika gereza la Quito ambako anazuiliwa.

Alikanusha mashtaka hayo, akidai alikuwa akifanywa mbuzi wa kafara kwa kuhusishwa na mauaji hayo.

Mshitakiwa mwingine Castilla, yeye alidaiwa kusambaza silaha, pesa na pikipiki kwa watu waliotekeleza shambulizi hilo.

Washitakiwa wengine waliohukumiwa ni Erick Ramirez, Victor Flores na Alexandra Chimbo, ambao walishtakiwa kwa kusaidia kikosi hicho.

Zaidi ya watu 70 walitoa ushahidi wakati wa kusikiliza kesi hiyo, akiwemo shahidi mkuu ambaye alisema genge hilo lilikuwa limepewa zaidi ya dola 200,000 za Kimarekani ili kumuua Villavicencio.

Mwanaharakati huyo aliyepinga ufisadi, alikuwa mmoja wa wagombea wachache ambao walidai uhusiano kati ya uhalifu na maofisa wa serikali unapanga uhalifu nchini humo.

**BBC**

## Chama cha Chilima chatishia kujiondoa serikali ya Malawi

**LILONGWE,** MALAWI

CHAMA cha aliyekuwa Makamu wa Rais wa Malawi, Saulos Chilima, kimetangaza kitajiondoa katika muungano unaounda serikali.

Hatua hiyo inatokana na madai yaliyotolewa na viongozi wa chama hicho kuwa mazingira ya kifo cha Chilima yanatatanisha.

Chilima alifariki mwezi mmoja uliopita akiwa na watu wengine wanane wakati ndege yao ya kijeshi, ilipoanguka katika msitu wa Chikangawa, karibu na mji mkuu wa Mzuzu.

Chama chake, United Transformation Movement (UTM) ni miongoni mwa vyama vinavyounda serikali ya nchi hiyo ikiongozwa na Lazarus Chakwera.

Taarifa ya chama cha UTM ilieleza kutoridhishwa na utawala wa MCP.

"Barua ya makubaliano ya muungano vimedhoofishwa na kusalitiwa na wenzetu, uwepo wa makubaliano hayo umekataliwa." " ilisema taarifa ya UTM.

UTM ilikuwa imeomba kufanyika kwa uchunguzi kuhusu ajali ya ndege siku chache baada ya kifo cha Chilima.

"Matukio ya kushangaza yanayohusiana na ajali ya ndege, jinsi habari inayozunguka tukio hilo ilivyoshughulikiwa na usimamizi wa juhudi za utafutaji na uokoaji inaacha nafasi kubwa ya uvumi," chama hicho kiliongeza.

Ndege ya kijeshi iliyombeba makamu huyo wa rais wa zamani ilitoweka baada ya kushindwa kutua Mzuzu kutokana na hali mbaya ya hewa, na kuamriwa kurejea mji mkuu wa Lilongwe.

**RF**

## MAKALA

# MAMBO YA FARAGHA SASA HADHARANI



Na Magabilo Masambu

**Mfano, umetuma cheti RITA kihakikiwe, tunatakiwa kujua kama kimepokewa, pili kila hatua mteja aone ili kuondoa wasiwasi kuhusu kushughulikiwa kwa tatizo lake.**

TAIFA lolote lisilojengwa katika misingi ya maadili mema ni rahisi kupoteza heshima yake. Ujenzi wa taifa huanza katika ngazi ya familia. Tunapoanza kulalamika dhidi ya maadili ya ovyo kwa baadhi ya watu katika nchi, hakuna namna tunaweza kukwepa lawama hizo.

Kwa jinsi tulivyo hivi sasa na huko tuendako itakuwa vigumu kufahamu mtu mzima ni yupi na mtoto ni yupi. Utu uzima au utoto hauwezi kupimwa kwa kigezo kimoja tu cha umri, bali matendo yetu. Kuna wakati mtu mzima anaonekana mtoto na mtoto anaonekana mtu mzima kutokana na matendo yake kwa jamii.

Kumezuka tabia ambayo tusipokuwa makini, taifa hili linakwenda kuangamia kabisa katika suala la maadili na utamaduni wetu. Kumezuka tabia ya baadhi ya watu wanaojiita wataalamu wa kutoa elimu mbalimbali kupitia majukwaa ya mtandaoni kuweka hadharani mambo ya faragha.

Si jambo baya kutoa elimu kwa jamii, lakini ni lazima kuzingatia aina za elimu tunayotoa kulingana na aina ya watazamaji, wasikilizaji na wasomaji wetu.

Kwa utamaduni wetu yako mambo ilikuwa ni vigumu sana kuyatamka hadharani iwe unafundisha au la! Lakini, siku hizi mambo hayo yanatumika kama viunganishi vya sentensi, yanatajwa bila kujali ni nani atakuwa mtazamaji na msikilizaji.

Yale yanayofanyika katika vitendo, sasa yanatamkwa kwa maneno bila woga kabisa na tunatazama, kisha tunajipigia makofi kwa elimu nzuri. Ndiyo ni elimu nzuri, lakini kwa nani?

Kwa watu waliopata angalau elimu ndogo tu ya masuala ya uandishi wa habari na utangazaji wanajua kwanini aina ya vipindi fulani unaweza kuvisikiliza wakati maalum na visiwe wakati wowote, zipo sababu na mojawapo ni kulenga hadhira inayokusudiwa.

Wako watu wanajiita makungwi, nadhani kama ni taaluma muhimu sana na watu wanaipenda, basi kuna umuhimu wa watu hao kujisajili ili watambulike rasmi kama walimu wa kuimarisha ndoa za watu, hata kama za kwao zimewashinda na wawekewe utaratibu wa namna ya kutengeneza maudhui yao yaweze kuwafikia walengwa bila kuathiri kundi lingine lisilokusudiwa.

Elimu hii wanayotoa si mpya, ilikuwapo, lakini ilikuwa na utaratibu wake na ilizingatia makundi husika. Ni kweli kwamba hata siri za unyago na jando wanaozijua ni wale waliokwenda na hiyo ndiyo ilikuwa heshima yake. Tumepumbazwa na hii dhana kwamba kila kitu kiwe wazi ili kujua hivi na vile lakini lazima tufahamu kwamba elimu inayotolewa kwa asiyehusika hugeuka sumu badala ya kumsaidia.

Kibaya zaidi, wako walioshindwa ndoa kwa matatizo yao wenyewe na wanatumia uzoefu huo kufundisha watu wengine kuwa kama wao, maana yake wanaongeza matatizo katika jamii kuliko kuyapunguza.

Vilevile, wanawake ndiyo walengwa wa elimu na kwa kiasi kikubwa inadhalilisha mwanamke, baadaye wanalalamika kwamba wanawake wanadhalilishwa.

Majukwaa ya mtandao hayana mipaka, hayachagui nani atazame nani asitazame, unaweza ukadhani kwamba watoto wako hawatazami kumbe mnatazama wote kwa pamoja, tofauti ni vifaa vinavyotumika kutama na kusikiliza, pia eneo la kutazama maudhui hayo.

Isivyo bahati, baadhi ya maneno hayo yanazungumzwa hata na baadhi ya viongozi wa dini kwa kujificha kufundisha ndoa, lakini waumini wao unakuta si wote wanandoa na wala hawatarajii kuingia kwenye ndoa hivi karibuni. Kanisani ambako tungetegemea lifundishwe neno la Mungu, panageuka kuwa ukumbi wa "kitchen part", kwanini yasiwapo mfunzo rasmi katika eneo rasmi kwa watu rasmi?

Yeyote anayetaka kutengeneza maudhui ya mtandaoni, lazima atafakari iwapo hayo maudhui yake anaweza kuyasikiliza yeye akiwa na watoto wake. Kama akijiridhisha anaweza basi ana haki ya kupakia mtandaoni.

Kwa upande wa serikali na watanzania kwa ujumla tunao wajibu wa kulinda maadili yetu kama taifa. Tuwaache watoto wasome, hayo tunayowafundisha sasa yataharibu mwelekeo wa maisha yao na baadaye tutawalaumu kwa kukosa maadili wakati sisi wenyewe tumeshiriki kuwaharibu na mwisho tunasema kizazi hiki ni cha namna gani.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Uongo wanaume kuwanasa wanawake kimapenzi huu hapa*



Na Adam Fungamwango

**Tuaanza na Pendo wa Bima Lee unaanza kwa mwanaume kulalamika kwa uchungu kuondoka kwa mpenzi wake Pendo na roho imenyong'onyea. Binti hataki kuvaa mitumba na kumwambia mpenzi wake heshima itashuka.**

INAELEZWA eti tangu enzi la mababu kuwa mwanaume akimpenda mwanamke uongo ni lazima utumike japo kidogo.

Wengine wakaenda mbali zaidi na kusema kama 'hukumpiga kamba' mwanamke huwezi kumpata, unachotakiwa ni kudanganya kidogo tu kwa ajili ya kushawishi kama vile mwanasiasa anavyoomba kura, ambapo wakati mwingine kile anachoahidi kwa mpigakura wake hawezi kukitekeleza.

Kwanza kabisa ieleweke kuwa uongo ni dhambi. Na binadamu hatakiwi kusema uongo kwa njia yoyote ile.

Unaweza kuongea uongo duniani ukafanikiwa kupata unachokihitaji, iwe mpenzi, mke au mali, lakini ni vya hapa duniani, mbele ya safari ni hasara kubwa.

Lakini pia kwa uchunguzi wangu tu mdogo nimegundua kuwa uongo kwa wanaume kuwadanganya wanawake kwa lengo la kuwashawishi wawakubali unaanzia miaka ambayo binadamu walishaanza kutawanyika kwenda kutafuta maisha sehemu nyingine na si zile karne za watu wanaozaliwa hapo hapo kijijini na kufia hapo bila kufika hata makao makuu ya mkoa.

Hawawezi kudanganyana kwa sababu wote wamezaliwa hapo hapo, hivyo si rahisi kumdanganya yeyote.

Wote wanafahamiana tabia, wazazi, uwezo, ukoo wao na kila kitu

Dunia ya sasa ya utandawazi kuna changamoto kubwa kwenye ndoa kwa sababu, hakuna anayemfahamu mwenzake vema.

Kila mtu anaficha 'makucha' au tabia mbaya aliyonayo isionekane mapema kwa mwenzake. Na huwa wanaoana kwa muda mfupi tu. Tabia zinaanza kuonekana ndani ya ndoa.

Kuna uongo fulani unaofanana na ukweli unaweza kuutumia kwa msichana ili kuweka mazingira mazuri, lakini mwingine baadaye unamdhalilisha hata aliyeutumia.

Unaweza labda ukamwambia msichana nina nyumba ili akukubali, lakini kumbe nyumba ya familia au ya urithi na siyo ya kupanga.

Unaweza kumwambia msichana kama una kazi umeajiriwa, lakini kumbe ni kibarua tu. Kwa sababu unapata pesa na unamudu maisha angalau, basi yeye ataamini kuwa una kazi ya kuajiriwa.

Tatizo ni pale unadanganya kuwa wewe ni mkurugenzi au meneja, wakati hata kazi yenyewe au kibarua tu huna, hili ni tatizo kubwa.

Bendi kadhaa ziliwaona watu wa ina hiyo na kutunga nyimbo ambazo ziliwaonya wanaume hao na kuwatahadharisha mabinti kuhusu watu wa aina hiyo, hivyo wawe makini.

Tuanze na Pendo wa Bima Lee unaanza kwa mwanaume kulalamika kwa uchungu kuondoka kwa mpenzi wake Pendo na roho imenyong'onyea. Binti hataki kuvaa mitumba na kumwambia mpenzi wake heshima itashuka.

"Pendo mimi mumeo kazi yangu ni kibarua wa kuponda kokota hapa mjini masikini eee, aaa Pendo.

Elimu ya ngumbaru, kisomo cha mwembeni, kisomo changu cha ukubwani, pesa nitazipata wapi? "

Mwanaume analalamika juu ya kuondoka mpenzi wake, akimueleza ukweli kuwa maisha na elimu yake ni duni.

Hapa hivyo ni kweli alimwambia hivyo mapema wakati anamtongoza?

"Usinambie chochote mume wangu, ulipokuja kwetu kunioa ulikuja na gari la fahari, na kusema wewe ni mhasibu mjini. Tena una miradi ya kufuga kuku na nguruwe, itakuwaje leo uniambie ni mponda kokoto?"

Mke anakumbuka alivyoingizwa 'mkenge' mwanzoni, lakini alipofika mjini akakuta ni tofauti, hivyo akakasirika.

"Sura yako nzuri na umbile lako nzuri ndilo lililosababisha nikudanganye, lakini mpenzi ukumbuke tangu zamani mwanaume akimpenda mwanamke, uongo ni lazima usemwe japo kidogo." Hapo mume anajitetea.

Huu ni uongo wa kiwango cha lami. Unafanana kabisa na ule ya 'Karubandika' wa Maquiz Original.

"Kaka wewe ungenipenda, kwa nini kunidanganya bwana we, kujibandika madaraka siyo yako bwana wewe, nimesikia tetesi kuwa huna lolote hata kazi huna ee, unazurura mchana kubwa kupita kurandaranda mitaani, kumbe hukuwa na uwezo wa kuniona ila kuniharibia maisha, heri kunieleza ukweli kuliko kunidanganya, nikuelewe vipi, babu ee uaminifu wako uko wapi ee, bwana.

Usinione bwege baba, kwa kukubali wito wako Karubandika, hayo yote ni matatizo ya dunia baba. Nilitaka kujitumbukiza ndani ya moto, kumbe bwana yule hana kitanda wala shuka, pa kulala hana analala kwenye stendi ya basi, na kituo cha Uda.

Akiingia kwenye baa kazi yake kuomba bia, hana hata aibu sigara pia aomba, mitaani na kwenya mastoo hujitangazia kuwa yeye ni Mkurugenzi wa Kampuni fulani, kumbe sivyo hivyo."

**Tuma meseji 0716 350534.**

# HADITHI

## Aka Simtaki-2

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda. Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka. Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ENHEE nani tena unataka kumuoa? Wa hapa hapa kijijini au?" Bi. Rehema akauliza maswali mawili kwa wakati mmoja.

"Hapa hapa kijijini!" Akajibu huku akitabasamu. Lilikuwa jibu moja. Mama akasubiri jibu la pili. Shukuru hakutaka kusema aliangua kicheko. "Niambie basi baba." Akabembeleza.

"Shani!" Akajibu kwa sauti ya upole. Mama akamuangalia kwa makini usoni mwanaye. Halafu akamwabia "Mhh, mwanangu nikasichana kazuri sana kale. Kwani vipi si kamemaliza shule kidato cha nne, hakaendelei?" "Hapana, wazazi wake wameshindwa kumuendeleza, kasema yeye yupo nyumbani tu." "Sawa, lakini baba yake wewe unamuoneje?" "Kwani yukoje mama?" "Mzee mkorofi na mtata yule, sijui kama mtawezana. Vizuri lakini mwanangu umechagua msichana mzuri, ana heshima na adabu. Mimi kama mama yako nitajitahidi kusukuma kupiga ndogo ndogo kwa mama yake ili barua tutakayoipeleka ikubaliwe."

"Ndiyo ninachokupendea hicho mama." Shukuru akasema huku akimkumbatia mama yake.


"Baba je sasa?" "Huyo niachie mimi. Ila kwa hili sidhani kama atapinga."

"Sawa mama hilo ndilo nililokuitia huku pembeni tutete, fanya kweli basi mama nakuamini, mimi natoka kidogo, nikirudi lazima nikuletee samaki kwa furaha yangu kesho tupike na ubwabwa."

"Haya mwanangu, umekuwa sasa baba." Bi. Rehema aliamuangalia kijana wake wakati anaondoka nyumbani hapo. Alipofika hatua kadhaa mbele, aligeuka nyuma na kukuta bado mama yake amesimama pale pale anamtazama. Akamuonyesha ishara kwa dole gumba, kuwa anamkubali na kumpenda sana mama yake.

******************************

"Nimebadilisha mawazo Kibwana!" "Nini Fotu?" "Nasema nasema nimebadisha mawazo yangu!" "Kwanza hebu niambie mawazo gani?" "Ya kuoa!" "Kumuoa Nyendo?" "Ndiyo, sitaki tena, nimeghairi!" Kibwana akashangaa kwa sekunde kadhaa akawa anamtazama Fotu usoni. Awali alidhani anafanya mzaha. Lakini kila alivyomuangalia hakuonekana kufanya masihara. "Kwa nini umeghairi, umemfumania, maana tayari umeshaniambia kuwa utamuoa na mimi ndiyo umeniambia nitafute mshenga mtu mzima kidogo aende kwao kupeleka barua."




**"Nimempata mwingine!" Jibu likamshtua Kibwana. "Unajua mimi sikuelewi Fotu, ni mzima kweli wewe?" "Mimi mzima kama chuma cha Mjerumani, sina malaria wala mafua, naongea nikiwa na akili timamu!" Bado mshangao uliendelea kujionyesha wazo machoni kwa Kibwana.**

"Kibwana ni kwamba yote yale niliyoyafanya nimeyasitisha kwa sasa." "Ndiyo kwa nini sasa?"

"Sijamfumania na wala hajanifanya kitu chochote." Fotu akajibu swali la Kibwana. "Sasa kumbe!"

"Nimempata mwingine!" Jibu likamshtua Kibwana. "Unajua mimi sikuelewi Fotu, ni mzima kweli wewe?" "Mimi mzima kama chuma cha Mjerumani, sina malaria wala mafua, naongea nikiwa na akili timamu!" Bado mshangao uliendelea kujionyesha wazo machoni kwa Kibwana.

"Ni hivi Kibwana, wala nisizunguke, nimeahirisha kumuoa Nyendo nimepata msichana mwingine!" Kama alidhania jibu hilo lingemfanya Kibwana kuacha kushangaa, alikosea. Ni kwamba lilizidisha.

"Unasemaje?" "Habari ndiyo hiyo!" "Yaani wewe Fotu leo ndiyo wa kusema hivyo wakati ulikuwa hadi unalia kuomba tukubembelezee Nyendo akubali!" "Nashukuru sana kwa kufanikisha hilo, lakini ndiyo hivyo, nimeamua kuchana na mpango huo." Kibwana alishusha pumzi kwa nguvu.

Walikuwa amekaa chini ya mti mkubwa wa mkuyu, katika kijiji cha Mtapenda, kilichopo maeneo ya Ugalla, kwenye mpaka wa mikia ya Tabora na Katavi.

Kilikuwa ni kijiji cha tatu baada ya Lalangulu anakoishi msichana Shani.

Fotu, kijana aliyezaliwa na kulelewa na wazazi ambao kwa maisha ya vijiji vile vya jirani, wao walikuwa moja ya watu wachache wenye uwezo.

Wakati wengi wa wanaoshi kwenye vijiji vile walikuwa ni wakulima na wafugaji, baadhi yao wakiwa pia vibarua waliohamia kutoka mikoa mingine, baba yake Fotu alikuwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kazamoyo na mama yake alikuwa karani kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Kutokana na hali hiyo, wahawkuwa hohe hahe kwani walikuwa na mishahara ambayo iliweza kuwafanya wajenge nyumba kubwa nzuri kuliko karibuni zote katika zaidi ya vijiji kumi vya Ugalla.

Nyumba kubwa safi ya bati la vigae, iliyonakshiwa na madirisha ya vioo, viliifanya kuonekana pambo kwenye kijiji kilichokuwa na nyumba nyingi za udongo zilizoezekwa makuti, zipo za udongo zilizokuwa na mabat chakavu, na chake mpya, vile vile kulikuwa chache zilizojengwa na saruji. Nyingi kati ya hizo matofali yake yanaonekana dhahiri kwa kutopigwa pasta au lipu. Zipo pia zilizojengwa kwa matofali ya udongo.

Wazazi wa Fotu na familia yao waliishi maisha bora, kwani pamoja na kuweza kujimudu kwa kuwa na mishahata kwa mume na mke, pia alinunua mashamba mawili makubwa ambayo walikuwa wanalimisha kwa trekta, au kuajiri vibarua kutokana na kumudu kulipa.

Walipata mazao mengi ya chakula na biashara hivyo kuwa na uwezo mkubwa, tofauti na wanakijiji wengi ambao baadhi yao hawakumudu hata kukodisha vibarua, achilia mbali trekta.

Waliendesha maisha yao kwa wao wenyewe na familia zao kwenda shamba kulima, huku wengine wakiwa ni vibarua waliokuwa wakikodishwa ambapo nao walikuwa wameshaoa na kutengeneza familia zao. Hayo ndiyo maisha si ya kijiji cha Mtapenda tu na Lalangulu, bali vingi nchini.

Kutokana na kuzaliwa na kulelewa kwenye maisha bora, Fotu alikuwa na kiburi na kuweza kufanya chochote anachotaka bila kumuogopa yoyote.

Alitembea na msichana yoyote anayemtaka kuanzia kijijini kwao mpaka na vya jirani. Hakupata shida sana kutokana na uwezo na umaarufu wa wazazi wake mbele ya wasichana ambao walitoka kwenye maisha duni.

Mara chache hutokea kuonekana uwezo au pesa si kila kitu kwenye maisha kwani hujikuta ameangukia kwa baadhi ya wasichana wenye misimamo, hali ambayo huwa inamuumiza mno, wakati mwingine kutaka kutumia nguvu au kulazimisha, lakini inashindikana.

Na hii ilitokea alipomtaka msichana wa hapo hapo kijijini kwao, Nyendo. Alikuwa msichana mrembo, lakini ulionekana kufifishwa na uwezo duni wa wazazi wake.

Pamoja na tabia yake ya kutembea na wanawake wengi, lakini moyo wake uliangukia kwa Nyendo.

Fotu aligonga mwamba kwa binti huyo, licha kumpa zawadi mbalimbali, kumhonga pesa ambazo alikuwa akizikubali, lakini hakufanikiwa kuwa naye. Mwishowe alianza vitisho kwa msichana huyo ambaye aliamua kukimbilia polisi. Kitendo cha yeye kuitwa polisi na kuonywa mbele ya wazazi wake na wa Nyendo kulimfanya anyong'onyee. Hata hivyo moyo wake uliendelea kuwa kwake. Kwa muda mfupi tu akaacha mbwembwe zake zote, kuchukua ovyo wasichana, badala yake aligauka kuwa mnyonge, aliyependa kukaa peke yake na kukaa kimya.

Hali hiyo iliwatisha wazazi na baadhi ya rafiki zake wachache, mwisho aliwatuma kwenda kwa Nyendo wambembelezee akubali kuwa wake na kuahidi kumuoa.


Jibu lililotoka kwa msichana huyo ni kwamba amekubali, lakini kwa sharti ya kutokuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi mpaka watakapofunga ndoa.

Hapo ndipo ugomvi ulipomalizika na wakawa wanakutana na kuzungumza, kila mmoja akiahidi kuwa mwangalifu mpaka pale watakapotimiza ahadi.

Ingawa hakuna yoyote aliyekwenda kumwambia mzazi wake, lakini tetesi zilianza kuenea kijijini hapo kuwa Fotu anataka kumuoa Nyendo.

**Itaendelea Jumapili**

HABARI BURUDANI




# WILLY PAUL SIO MAJIGAMBO HAYO!

MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Willy Paul, amejigamba kuwa yeye ndiye msanii pekee kutoka nchini humo muziki wake unapendwa nje ya mipaka ya ukanda wa Afrika Mashariki.

Willy amechapisha ujumbe katika ukurasa wake wa Instagram, akisema kila siku anawaombea wanamuziki wenzake kufanya juhudi ili ngoma zao zipenye nje ya mipaka ya Kenya.

"Wasanii wa Kenya wanastahili kutia bidii na juhudi kama Pozee, ndio msikike nje ya Afrika Mashariki kama Pozee. Sijui ni kwanini ni mimi tu msanii kutoka Kenya ambaye nyimbo zake zinavuma nje? Mungu bariki na wengine pia aaa! Lakini usipunguze Baraka za kwangu," ameandika Willy Paul.

# Coy Mzungu atamani kumiliki nyumba zaidi

MSANII wa uchekeshaji, Coy Mzungu, amesema jengo la ghorofa analojenga linatokana na pesa ambazo zinatokana na zaidi ya sanaa anayoifanya.

Amesema jengo hilo halitakuwa la kuishi na familia yake, bali maalum kwa ajili ya biashara mbalimbali kwa lengo la kujiongezea kipato.

"Nyumba yangu ya kuishi bado sijaifikiria, hili jengo litakuwa la biashara pekee kwa sababu lazima niweke malengo yangu ya baadae. Nimefurahi kuona jambo hili linafikia mwisho na kupata ndoto yangu," amesema.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ZIRKZEE FRESH MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imekubaliana maslahi binafsi na mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee na wako kwenye mazungumzo na Bologna kuhusu jinsi klabu hiyo ya Italia inataka kima cha ya kuachiliwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(CaughtOffside)***

### LUKAKU KUMPISHA OSIMHEN

CHELSEA iko tayari kuwatoa mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31, na kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 21 kwa Napoli ili kusaidia kupunguza bei ya mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25. ***(Teamtalk)***

### BADO KWA CALAFIORI

ARSENAL bado haIjafikia bei ya Bologna ya pauni milioni 42.3 kwa ajili ya kumnunua mlinzi wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22, na mazungumzo kati ya klabu hizo mbili yanaendelea. ***(Football Italia)***

### ATAKIWA MILAN

AC Milan imetoa ofa ya awali kwa beki wa kulia wa Tottenham Hotspur na Brazil, Emerson Royal lakini kuna pengo kati ya tathmini ya klabu kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Sports Italia)***

### GROSS HUYO DORTMUND

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Pascal Gross amekubali maslahi binafsi na Borussia Dortmund, ambao wako kwenye mazungumzo ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 kutoka Brighton kwa kati ya pauni milioni 6. ***(Sky Sports Germany)***

### GALLAGHER ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imehusishwa na kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher mwenye umri wa mkaka 24, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa England hana uwezekano wa kuhamia Spurs msimu huu wa joto.***(Football Insider)***

### ALMIRON KUHAMIA SAUDIA

WINGA wa Newcastle United, Miguel Almiron yuko kwenye mazungumzo na mwakilishi wake kuhusu mustakabali wake huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Paraguay mwenye umri wa miaka 30 akihusishwa na kuhamia Saudi Arabia na Magpies wanaaminika kuwa tayari kumuuza. ***(Chronicle)***

### KUBAKIA ATLETICO MADRID

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Alvaro Morata anatafakari iwapo ataondoka Atletico Madrid na kujiunga na AC Milan, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 akisema atasalia katika klabu hiyo ya Hipania hadi ashinde nao kitu. ***(Corriere dello Sport)***

### AGOMBEWA BARCA, MADRID

REAL Madrid ina imani kuwa inaweza kuwashinda wapinzani wao Barcelona katika kumsajili kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa miaka 21. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# BARCELONA WAKARIBIA KUMSAJIILI WILLIAMS

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa LaLiga, Javier Tebas amesema kuwa Barcelona wanakaribia kumudu usajili wa winga wa Athletic Club, Nico Williams.

**Williams mwenye umri wa miaka 22, ana kipengele cha kuachiliwa kwa euro milioni 58 katika mkataba wake na rais wa Barca, Joan Laporta alisema wiki iliyopita klabu hiyo ya Katalunya inaweza kumudu kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania.**

Barca wamesalia kuvuka kiwango cha matumizi ya kila mwaka kilichowekwa na LaLiga, na kuwazuia kusajili wachezaji wapya, lakini Tebas alisema hali yao ya kifedha imeimarika.

● ● ● Nyota huyo wa Athletic Club ana kipengele cha....

"Ikiwa Barça itarejea kwenye kikomo cha matumizi cha 1:1 ikiruhusiwa kuweka chochote wanachoongeza katika uhamisho au akiba kwenye mishahara, kumaanisha kwamba hawazidi kiwango chao cha juu, wataweza kufanya hivyo," alisema Tebas akiiambia Diario Sport alipoulizwa kama dili la Williams litawezekana kifedha.

"Lazima ufikirie kwamba kwa juhudi za Barcelona kupunguza bili yao ya mishahara kwa zaidi ya Euro milioni 200 na hatua zingine ambazo tayari zimefanyika ndani ya klabu ambazo hazihusiani na wafadhili wao wa kifedha inawezekana kabisa kuleta mchezaji kama Nico Williams.

"Nadhani ana kipengele cha euro milioni 58. Unapomsajili mchezaji kwa euro milioni 58, malipo yanagawanywa na miaka ya mkataba; ukimsajili kwa miaka mitatu, itakuwa chini ya euro milioni 20 kwa mwaka.

"Barça wataweza kuwa karibu na kiasi hicho, ambacho kinakubalika kabisa ikiwa watarudi ndani ya sheria ya 1:1.

"Ni klabu ambayo inakaribia euro bilioni 1 kwa mauzo, wanaweza kuwa katika safu hiyo kwa aina hiyo ya usajili.

"Lazima tukumbuke kwamba hali ya 1:1 lazima itimizwe kwanza, ingawa. Bado hawapo, lakini ni wa karibu zaidi. Wakifika hapo, wanaweza kumsajili Nico Williams au mchezaji mwingine mwenye sifa hizo. "

# FAINALI YA KIBABE ENGLAND VS HISPANIA LEO



**BERLIN,** Ujerumani

ENGLAND imepata bahati yao zaidi ya mara moja katika michuano hii ya Ulaya na leo Jumapili watamenyana na Hispania kwenye Fainali ya Euro 2024.

Hii ni baada ya kuwanyamazisha wakosoaji wao kwa kufuzu fainali kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Uholanzi Jumatano iliyopita.

'Simba Watatu' hao walilala 1-0 baada ya dakika saba tu katika mchezo wa nusu fainali dhidi ya Uholanzi, lakini mkwaju wa penalti wa Harry Kane na ule wa dakika za mwisho kutoka kwa Ollie Watkins uliipeleka England katika fainali ya pili mfululizo ya Euro.

Inayowasubiri itakuwa timu yenye nguvu zaidi katika michuano ya mwaka huu, Hispania, ambayo iliitoa Georgia, Ujerumani na Ufaransa katika hatua ya mtoano na kufuzu kwa fainali ya kesho.

**Habari za timu**

Mabeki Robin Le Normand na Dani Carvajal wanatazamiwa kurejea kutoka kwenye adhabu ya kufungiwa kwa Hispania, lakini Pedri bado yuko nje kwa hivyo Dani Olmo atachukua nafasi yake katika safu ya kiungo.

Kocha Gareth Southgate anaweza kuchagua kumbadilisha Kieran Trippier upande wa kushoto na kumchukua Luke Shaw.

**Takwimu**

Hispania wameshinda mechi zote sita za Euro 2024 bila kuhitaji mikwaju ya penalti na pia ndio wafungaji bora wa michuano hiyo wakiwa na mabao 13.

England imebanwa sare katika muda wa kawaida katika mechi nne kati ya tano zilizopita na kufungwa katika mechi tatu zilizopita dhidi ya Slovakia, Uswisi na Uholanzi.

# Sancho arudi Man United

**MANCHESTER,** England

JADON Sancho anatazamiwa kujumuishwa tena kwenye kikosi cha Manchester United kufuatia mazungumzo na kocha Erik ten Hag, chanzo kiliiambia ESPN.

Sancho hajaichezea United tangu Agosti baada ya kumkosoa hadharani Mholanzi huyo katika chapisho la mtandao wa kijamii.

Alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo katika klabu ya Borussia Dortmund na kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini baada ya kufanya mkutano na Ten Hag wiki hii, Sancho amerejea mazoezini na kikosi cha kwanza.

Hatasafiri hadi Norway kwa mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya na Rosenborg siku ya Jumatatu lakini atapatikana kwa mechi zijazo.

United itamenyana na Rangers huko Murrayfield mnamo Julai 20 kabla ya kusafiri kwenda Marekani Julai 24 kwa ziara ya mechi tatu.


Sancho alifukuzwa kwenye kikosi baada ya kukosana na Ten Hag kwa kile alichodai alidanganywa kuhusu sababu za kumuondoa katika mchezo wa kichapo cha 3-1 kutoka kwa Arsenal Septemba.

Ten Hag amesema mara kwa mara mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 hataruhusiwa kurejea hadi aombe msamaha.

United wamekataa kufichua ikiwa Sancho aliomba msamaha au la wakati wa mkutano wake na Ten Hag.

Klabu hiyo imekuwa tayari kutoa ofa kwa Sancho msimu huu wa majira ya joto huku Juventus ikiwa ni moja ya klabu zinazomtaka, lakini thamani yao ya pauni milioni 40 imeonekana kuwa na matatizo.

Taarifa iliyochapishwa kwenye tovuti ya klabu siku ya Ijumaa ilisomeka: "Jadon Sancho alirejea kufuatia muda wake wa mkopo Borussia Dortmund katika kipindi cha pili cha msimu uliopita."



# *Ni Argentina na Colombia Fainali Copa America*

**MIAMI,** Marekani

ARGENTINA wanawania taji la 16 watakapomenyana na Colombia katika fainali ya Copa America kwenye Uwanja wa Hard Rock, Miami Gardens, Florida, Marekami mapema Jumatatu Alfajiri.

Kikosi cha kocha Lionel Scaloni kilishinda Copa America 2021 na Kombe la Dunia la 2022 na wanatumaini kupata taji kuu la tatu katika miaka mitatu.

Hata hivyo, watakuwa wakitarajia changamoto kali kutoka kwa Colombia, ambao wanarekodi ya kucheza mechi 28 bila kushindwa.

Colombia wameshinda mechi 12 kati ya 13 zilizopita isipokuwa sare ya 1-1 dhidi ya Brazil katika hatua ya makundi ya Copa America.

Hata hivyo, wametwaa ubingwa wa Copa America mara moja tu, mwaka 2001 na hawajawahi kushinda michuano hiyo katika ardhi ya kigeni.

**Habari za timu**

Beki aliyesimamishwa Daniel Munoz atakuwa pigo kubwa kwa Colombia.

Julian Alvarez alicheza mbele na Lionel Messi katika ushindi wa 2-0 wa nusu fainali ya Argentina dhidi ya Canada na wote wakapata bao.

Wanaonekana kushika nafasi zao kwa gharama ya Lautaro Martinez, ambaye ndiye mfungaji bora wa michuano hiyo akiwa na mabao manne.

Beki wa kulia wa Colombia, Munoz anatumikia adhabu ya kufungiwa mechi moja baada ya kadi nyekundu yake dhidi ya Uruguay, huku kiungo Richard Rios akitoka katika mchezo huo na nafasi yake kuchukuliwa na Mateus Uribe.

**Takwimu**

Argentina wameshinda mechi 17 kati ya 19 zilizopita.

Albiceleste hao wameshinda mechi tisa kati ya 25.

Argentina wamepoteza mchezo mmoja tu kati ya michezo 25 iliyopita huku chini ya mabao matatu yametua katika mechi zao zote tisa za mwisho za mashindano.

Colombia hawajafungwa katika mechi 28 zilizopita na wameshinda mechi 12 kati ya 13 zilizopita.

**Utabiri**

Colombia wameweka pamoja mkimbio wa ajabu wa michezo 28 bila kushindwa lakini wana rekodi mbaya dhidi ya Argentina, wakishinda mechi tisa kati ya 43.

Tangu Februari 2022 Colombia wameonja kichapo lakini washindi wao katika hafla hiyo walikuwa Argentina, ambao walipata ushindi wa 1-0 nyumbani katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia.

HABARI MICHEZO

## Gamondi: Nataka kuifanya Yanga

INATOKA UK. 24

vyema zaidi ya msimu uliopita kwenye michuano ya kimataifa, hii ni ngumu, ila nataka Yanga iwe ndani tano bora katika bara la Afrika na hili litatokana na ushirikiano wa Wanayanga wote, nasema najua ni ngumu kwa sababu huwezi kushinda kila mechi, lakini angalau kurudia matokeo tuliyoyapata huko nyuma karibuni kila msimu, ni vyema sana na inaweza kutufikisha huko," alisema Gamondi.

Yanga kwa sasa inashika nafasi ya 13 kwenye ubora barani Afrika, kwa mujibu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu barani Afrika (CAF) wakiwa na pointi 31, huku watani wa jadi Simba wakiwa kwenye nafasi ya saba kwa kujikusanyia pointi 39.

Kikosi hicho kwa sasa kipo mazoezini Kigamboni kikijiandaa na msimu mpya huku kikiwa kimewaongeza wachezaji kadhaa akiwemo Mzambia Clatous Chama aliyekuwa mchezaji wa Simba, Mzimbabwe Prince Dube aliyesajiliwa kutoka Azam FC, Mkenya, Duke Abuya na golikipa Mtanzania, Khomeiny Aboubakar, wote kutoka Singida Black Stars na Mkongomani Shadrack Boka kutoka FC Saint Eloi Lupopo kutoka DR Congo.

## Kocha Fadlu ataka Simba

INATOKA UK. 24

mipira wapinzani mara tu wanapoipoteza.

Akizungumzia siku za awali za mazoezi, alisema walikuwa na kazi kubwa kwanza ya kuzoea hali ya hewa na kufahamiana baina ya makocha na wachezaji.

"Kwanza tulikuwa na kazi ya kuzoea hali ya hewa, makocha wangu wa utimamu wa mwili wakaanza kufanya kazi, tulijaribu kuwazoea wachezaji na wao kutuzoea sisi, kikubwa nilitaka kujua aina ya wachezaji ninaofanya nao kazi, hii ndiyo hali tuliyokutana nayo siku za mwanzo, kidogo kidogo wataanza kupokea na kuyafanyia kazi maelekezo na mafundisho tunayowapa," alisema Fadlu.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi katika tamasha la 'Simba Day' ili waje kuona makocha na wachezaji wao wapya, pamoja na soka safi la kuvutia.

"Nawaomba wanachama mashabiki waje kutuona kwa mara ya kwanza, ni siku ya utambulisho wa benchi la ufundi ambalo ni jipya na wachezaji wao wa msimu ujao wakiwemo waliosajiliwa hivi karibuni, lakini pia waje kuona soka safi," alisema kocha Fadlu.

# TANZANIA PRISONS YAMSAJILI NYOTA WA ZAMANI SIMBA SC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imefanikiwa kunasa saini ya winga wa zamani wa Simba na timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Haruna Chanongo.

Mchezaji huyo amejiunga na kikosi hicho akitokea Pamba FC, ambapo alikuwa mmoja wa wachezaji tegemeo walioisaidia timu hiyo kupanda daraja kutokea Ligi ya 'Championship'.

Uongozi wa klabu hiyo ulithibitisha usajili huo jana kupitia taarifa yao rasmi ya klabu hiyo.

**"Karibu kwenye familia ya wajelajela kiungo na winga, Chanongo, kuanzia leo ni mali ya Prisons," ilisema taarifa rasmi ya klabu hiyo jana.**

Klabu hiyo imemsajili winga huyo mzoefu kwenye Ligi Kuu ya Tanzania Bara ili kukiimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao baada ya kulazimika kupambana sana kubakia Ligi Kuu msimu uliopita.

Chanongo alikuwa mmoja wa wachezaji waliopandishwa kwenye kikosi cha kwanza cha Simba kutoka kikosi cha pili cha timu hiyo mwaka 2012.

Aliichezea Simba hadi mwaka 2015 na kutimkia Stand United, hadi 2016 alipojiunga na Mtibwa Sugar ambapo aliichezea timu hiyo hadi mwaka 2022 alipokwenda Ruvu Shooting na msimu uliofuata akaenda kuichezea Pamba FC ikiwa 'Championship'.

Klabu hiyo pia imemsajili golikipa wa Geita Gold, Sebusebu Samson kwa ajili ya kuongeza nguvu eneo hilo.

Sebusebu ni mmoja wa magolikipa mahiri, ambaye alifungwa mabao machache kwenye Ligi Kuu licha ya timu yake ya Geita Gold kushuka daraja.




Wachezaji wa timu ya Kipera FC, Shabani Ramadhani (kushoto), na Mwita Marwa, wakiwania mpira kwenye mazoezi ya timu hiyo jana Uwanja wa Shule ya Msingi Kipera. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tenisi taifa waenda Botswana*

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya mchezo wa tenisi imeondoka jana asubuhi kuelekea Botswana kushiriki mashindano ya Dunia kanda ya tano yatakayoanza kesho mpaka Julai 20.

Akizungumza na Nipashe jana muda mfupi kabla ya timu hiyo haijaondoka, Makamu wa Rais wa Chama cha mchezo wa tenisi Tanzania (TAA), Rajabu Borri, alisema timu hiyo imeondoka na wachezaji wanne.

"Kwa sasa tunajiandaa kuelekea Botswana, tumelazimika kuwahi ili wachezaji wakazoee hali ya hewa pamoja na mazingira ya mchezo, alisema Borri.

Alisema kwa upande wao kama chama kwa kushirikiana na Serikali wameiandaa timu hiyo vizuri ili kuhakikisha inakwenda kuiwakilisha vema Tanzania.

Aidha, alisema mashindano hayo yatakuwa na ushindani mkubwa kwa kuwa yatashirikisha timu kutoka Mataifa mbali mbali hivyo amewataka wachezaji kucheza kwa tahadhari kubwa.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salum Mvita alisema hana wasiwasi na wachezaji wake kwani amewapa mbinu ambazo zitawasaidia kupata matokeo mazuri.

"Tumefanya maandalizi kwa kipindi kirefu kwa ajili ya kuipa heshima nchi yetu kupitia mashindano haya, tunaomba watanzania watuombee tutimize malengo yetu, alisema Mvita.

# Michezo

Jumapili Julai 14, 2024

Nipashe




Barca wakaribia kumsajili Williams UKURASA 21



Wachezaji wa timu ya taifa ya England, Kyle Walker (kulia) na John Stones wakiwa kwenye mazoezi ya mwisho jana kabla ya mchezo wa leo wa fainali ya michuano ya Euro 2024 dhidi ya Hispania. **PICHA: MTANDAO**

# Gamondi: Nataka kuifanya Yanga iwe tano bora Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Apanga kutengeneza kikosi tishio kuliko cha msimu uliopita ili...

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema anataka kutengeneza kikosi tishio zaidi kuliko cha msimu uliopita, huku lengo lake ikiwa ni kuifanya timu hiyo iingie kwenye timu tano bora Afrika.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, kocha huyo raia wa Argentina, aliyeiwezesha Yanga kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara msimu uliopita na kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, alisema pamoja na matamanio hayo bado wanatakiwa kufanya kazi ya ziada kufikia malengo hayo.

**Alisema malengo hayo yanaweza kufanikiwa kutokana na kuongeza baadhi ya wachezaji wenye viwango vikubwa kwenye usajili.**

“Kila mtu anajua aina yangu ya ufundishaji ni kucheza soka la kuvutia, kupata ushindi na mataji, lakini kuelekea msimu ujao tunataka kuwa bora zaidi kuliko msimu uliopita ingawa haitokuwa rahisi, kutakuwa na changamoto kubwa, huu ni ujumbe kwa mashabiki wote wa Yanga na wadau wa soka kuendelea kutuunga mkono msimu ujao, ya msimu uliopita yamepita, wajue msimu ujao tutapata changamoto kutokana na uwezo wetu mkubwa tuliokuwa nao huko nyuma, hivyo timu nyingi zitakuwa zimejiandaa kwa kusajili vizuri na kutengeneza nguvu ya kupambana na sisi, hivyo sisi tunatakiwa tuongeze ubora zaidi,” alisema kocha huyo.

Alisema pamoja na kwamba watakutana na ugumu, lakini na wao watakabiliana nao kwani wameongeza baadhi ya wachezaji wachache ambao wana uwezo wa hali ya juu hasa kwenye michuano ya kimataifa.

“Hatukutaka wachezaji wengi ndani ya kikosi chetu, bali wachache tu wenye ubora wa kutuongezea nguvu, tulitaka wale wazoefu wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika lengo ni kuendelea kutawala soka la Tanzania na kufanya

INAENDELEA UK. 23

# Kocha Fadlu ataka Simba itakayofunga mabao mengi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlur Davids, ameahidi kusuka safu kali ya ushambuliaji itakayokuwa tishio kwa timu yoyote itakayokutana nayo akitaka washambuliaji wake wafunge mabao mengi katika mechi moja.

Akizungumza jana kutoka Ismailia nchini Misri ambako kikosi cha Simba kimeweka kambi, amesema moja ya kazi ambayo ataifanya ni kutengeneza safu kali ya ushambuliaji kwa sababu kwake ni kazi rahisi kwani katika karia yake ya soka alikuwa mshambuliaji na amewahi kuwa mfungaji bora mara mbili nchini Afrika Kusini wakati akicheza soka.

Kocha huyo maarufu Afrika Kusini, ndiyo kwanza ameanza kukinoa kikosi cha Simba kuelekea msimu ujao wa mashindano, akichukua mikoba ya Abdelhak Benchikha raia wa Algeria aliyeondoka kabla ya Ligi Kuu ya msimu uliopita kumalizika.

“Nataka kutengeneza safu kali ya ushambuliaji, tunatakiwa kufunga mabao mengi ili kushinda mchezo wa mpira wa miguu, usipofunga utatoa sare, au utafungwa kabisa, ninachofanya ni kutengeneza muunganiko, maelewano, mikimbio ya kusaka nafasi, mawasiliano ya mdomo na mwili kwa washambuliaji wangu ili wafunge mabao mengi kama nilivyokuwa nafunga mimi, hata kuwafua vyema wale wanaotengeneza nafasi, viungo washambuliaji ambao nao watatakiwa kuwa na maelewano, kutengeneza mfumo wa kucheza kwa kuwahadaa mabeki, au kupiga mipira juu ya migongo yao ili kulisha washambuliaji ili wafunge kwa urahisi,” alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema hayo yote hayawezi kufanyika bila ya kuwa na msingi imara wa mabeki na viungo wakabaji ambao wana uwezo mzuri na kupora

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042